Tazama, Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa

Asante, Ndugu Borders.

2 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo sasa, kwa maombi. Ikiwa tuna haja zozote, na tumwinulie Mungu mikono yetu na kimyakimya, moyoni mwetu, tuseme, “Mungu, nikumbuke.”

3 Baba yetu wa Mbinguni, tumekusanyika, usiku wa leo tena, siku moja karibu zaidi na wakati ule mkuu ambapo Wewe utauvuta wakati uuingize katika Umilele. Tumekuwa na majaliwa ya kuishi leo, na kuona, wengi wetu, na kusikia, tukiwa na hisi zetu, tukimhisi Roho wa Mungu ndani ya moyo wetu. Tunashukuru kwa hilo. Usiku wa leo, kabla tu ya mkutano huu, mioyo imetiwa joto na mikono imeinuliwa. Matarajio, usiku wa leo, ni makubwa, Baba. Tusaidie sasa kupokea kile tunachoomba. Ninaomba ya kwamba utamtukuza Mwanao, Kristo, mbele ya wasikilizaji, usiku wa leo. Katika Jina la Yesu Kristo naomba. Amina.

4 Mwaweza kuketi. Ninyi ni kusanyiko zuri sana, na ni wazuri sana kuzungumzia, nimekuwa nikizungumza kwa muda mrefu sana, nikiwacheleweshа sana. Kesho alasiri ndiyo ibada yetu ya kufunga. Hakika ninaamini kwamba Roho Mtakatifu ametuthibitishia kwamba Yeye yuko hapa. Sasa, hebu tusukume kila kitu tuwezacho sasa, maombi. Na tuwe tayari, chochote alicho nacho kwa ajili yetu, kwamba tutakipokea.

5 Sasa, kuna wageni wengi hapa. Kuna wengine hapa kutoka sehemu zingine za nchi. Na sasa, asubuhi, hudhurieni shule ya Jumapili. Watu hawa hapa ni watumishi wa Kristo. Ni watu wanaoamini katika huduma ii hii ninayohubiri, wao ni wahudumu, watendakazi wenza, raia wa Ufalme wa Mungu, wana makanisa hapa, wangefurahi kuwa nanyi katika ninii yao . . . kesho asubuhi, kuhudhuria makanisa yao, kila mmoja.

6 Nanyi mwajua . . . Nadhani wametoa tamshi hilo, lakini sikuzote mimi husema hivi: Ni dhambi kuwatuma watoto wako kwenye shule ya Jumapili. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Ni dhambi kuwatuma watoto wako kwenye shule ya Jumapili; inakupasa kuwapeleka. Kwa hivyo hakikisha kufanya hivyo. Nenda pamoja na watoto wako, kesho, kwenye shule ya Jumapili. Watu hawa, labda, wameliweka kanisa lao katika hali nzuri lipate kushughulikia umri wowote, na watoto wote wadogo kwa wakubwa na *wote kadhalika*. Mtasikia Neno la Bwana.

7 Nami naomba ya kwamba kila moja la makanisa yao, kesho, litajazwa sana na Roho Mtakatifu mpaka ishara, maajabu, miujiza na kadhalika itatukia kanisani mwao, na kutakuwa na utukufu mkuu pamoja na heshima kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Ninaamini kwa moyo wangu wote.

8 Sasa, upesi, kuingia moja kwa moja kwenye ujumbe wa usiku wa leo. Nami ninataka kuwa na hakika sasa, kesho alasiri, nafikiri ni saa nane, ama saa nane na nusu, ama kitu kama hicho. Na ni kadi ngapi za maombi…? Je, tuna kadi nyingi za maombi nje? Tunapaswa kuwafanya hawa… Mwajua, hatuna budi kuwaombea. Kila mtu, anayepata kadi ya maombi, huombewa. Nao watakuwa wakisambaza kadi za maombi kesho alasiri, kama, loo, muda mfupi kabla ya ibada kuanza, ningesema angalau dakika arobaini na tano, ili wasiingilie ya—ya jioni, au, ibada ya alasiri. Kwa hiyo huyo mvulana atakuwa hapa, naye atakuwa na mtu fulani pamoja naye wa kumsaidia, nao watakuwa wakisambaza kadi za maombi yapata, labda nusu saa kwa vyovyote vile, ama labda zaidi kidogo, kwa mtu yeyote anayetaka kadi ya maombi. Nasi tutamwombea kila tuwezaye.

9 Nimekuwa nikijaribu sana, lakini, mkono wangu ukiwa juu ya Biblia, usiku wa leo, na kuna watu hapa pamoja nami ambao wanajua kwamba mikutano hii huku na huku pwani imekuwa mikutano ya majaribio. Ninaondoka kuelekea huduma za umishenari. Iwapo nitarudi tena, itakuwa ni ibada tofauti na zile nimekuwa nazo, nitawaombea wagonjwa pekee. Mnaona? Mimi… Ni… Upambanuzi hauendani na watu wa Marekani, watu wasomi, hawauoni, moja ya mambo hayo yanaweza kutokea Afrika na elfu ishirini na thelathini watakimbilia madhabahuni mara moja.

10 Lakini sisi kidogo tunafanana na… Mwanamke alionekana, nchini mwetu, katika duka la bei rahisi si muda mrefu uliopita. Alikuwa akijaribu kumwonyesha mvulana mdogo kila kitu ambacho kinapaswa kuuvutia umakini wa mvulana mdogo, na baada ya kitambo kidogo, angechukua kengele ndogo na kuzipiga, naye angekodoa macho tu, anaangalia tu. Basi hatimaye, huyo mama akalemewa, akaanguka tu kwenye kaunta.

11 Baadhi ya watu waliokuwa wamesimama pale wakamwendea na kutaka kujua ilikuwaje, alikuwa akilia, akasema, "Ni mvulana wangu mdogo." Akasema, "Siku moja aliketi tu, akaanza kuketi, amekodoa macho." Kisha akasema, "Hakuna kitu ambacho kinapaswa kuvutia mvulana mdogo, wa umri wake, kinachomvutia tena, anakodoa macho tu angani."

12 Hapo ndipo karibu kanisa limefikia, Mungu ametikisa kila karama ya kiroho inayoweza kutikiswa, ambayo imetajwa katika Biblia, mbele zao, nao wanakodoa macho tu. Vema, nadhani ni sawa, labda, nadhani ndivyo ilivyo.

13 Inanikumbusha juu ya mshairi mzee, Mwingereza—mshairi Mwingereza, nasahau jina lake. Alikuwa anaandika... Sikuzote, alipenda bahari, lakini hakuwa amewahi kuiona, kwa hiyo siku moja alikuwa akishuka kwenda baharini, akakutana na baharia mzee akitoka baharini, naye akasema, "Unakwenda wapi, rafiki yangu mwema?"

14 Akasema, "Ninaenda baharini," kasema, "Nimeandika habari zake, lakini sijawahi kuiona." Kasema, "Ninatamani kunusa mawimbi yake yaliyokifu chumvi, ningependa kuona mawimbi yake meupe yanapotokea, kusikia shakwe wa baharini wanaporuka."

15 Naye maskini huyo baharia mzee, akiwa na ndevu usoni mwake, akatoa kiko chake cha gunzi la hindi na kutema mate, akasema, "Nilizaliwa juu yake miaka sitini iliyopita, nimekuwa huko tangu wakati huo, sioni cha kusisimua juu yake."

16 Ni kitu gani? Alikuwa ameiona sana hadi ikawa kawaida kwake. Hiyo ndiyo shida yetu sisi Wapentekoste. Tumeona utukufu mwingi sana wa Mungu hadi umekuwa wa kawaida kwetu, hautusisimui tena.

17 Nimejaribu sana. Huu ndio mkutano wangu wa kufunga wa Marekani. Hakika, nilijisikia kuja hapa kwenye nchi hii. Nililipeleka kundi hili la watu wazuri, hivi majuzi asubuhi, kwenye kifungua kinywa, wala sijapata kukutana na kundi la watu wazuri namna hii, watu wowote bora zaidi maishani mwangu, watu halisi wa Roho, mioyo iliyojaa upendo kwa watu wao, wao ni wachungaji, wachunga kondoo.

18 Hamjui vita, ambavyo watu hawa wamevipiga, kuuleta mkutano huu hapa. Hiyo ni kweli. Lakini wanautaka mbele za watu wao, wanataka watu wao wakue katika neema ya Mungu, nao wanajaribu kuwafanya wajue zaidi kumhusu Mungu. Nao wanaposikia jambo fulani la Mungu, wakalichunguza na kuwazia ni la kweli, wanalileta mbele ya watu bila kujali itawagharimu nini. Nina heshima na staha kwa watu kama hao. Hiyo ni kweli.

19 Na tumekuwa na kuwekeana mikono mikutanoni, tumekuwa na hilo tangu, miaka na miaka na miaka na miaka. John Wesley aliwaombea wagonjwa, Calvin, Knox, Spurgeon, wote kote kote, waliwaombea wagonjwa na kuweka mikono juu ya wagonjwa. Ikaja Pentekoste pamoja na kunena-kwa-lugha na tafsiri, na kadhalika, na kuendelea, lakini kamwe hatujawahi kuona kile Roho Mtakatifu anatufanyia sasa hivi. Mnaona?

20 Na hilo ndilo ninalojaribu kuwaelezea watu, kwamba hamna haja ya kungoja hadi karama fulani maalum ipitie nchini, Kristo yuko pamoja na Kanisa Lake daima. Vipi kama ungekuwa umelala hapa nje, barabarani, ukivuja damu vibaya sana katika ajali? Kisha useme, "Sina budi kutuma mtu, kumleta Ndugu Branham, Ndugu Roberts, ama mtu fulani, aje aniombee"?

Kristo yuko papo hapo, yuko daima. Unaona? Hilo ndilo ninalojaribu kuwafanya watu waone, lakini baada ya ziara baada ya ziara, kote nchini, bado linabakia vile vile.

21 Na kadiri nijuavyo, isipokuwa Mwenyezi Mungu anifunulie kufanya vinginevyo, huu utakuwa ndio mkutano wangu wa mwisho Marekani, Majimbo ya Marekani, chini ya upambanuzi, sikuzote nitahubiri na kuwaombea wagonjwa. Nikienda katika nchi zingine, nitatumia huo. Kwa sababu hamjui, kamwe hamtajua kile huo unachonifanyia, unanidhoofisha, ono moja litanivuruga kwa muda mrefu kuliko . . . zaidi ya kusimama hapa kwa saa tatu nikihubiri. Nami hufanya hivyo, nikipumzika ili kuona kitakachotokea, na ni . . . halichukui tu, hivyo tu.

22 Nilisimama Afrika Kusini, alasiri moja, nikiwa na yapata kati ya . . . yapata watu laki mbili, jukwaa, kitu kama hiki, lililojengwa ambapo uwanja wa mashindano ya mbio . . . Ilinibidi kuijenga upande huo mwingine wa uwanja wa mashindano ya mbio, nikasimama pale, hakuna njia ya kusambaza kadi za maombi, kulikuwa tu na maelfu mara maelfu. Hatukuwa na mtu . . .

23 Nikawatuma wamishenari, "Shukeni mkamlete mtu mmoja kutoka kwa makabila yenu mnayohubiria." Wakawapanga kundi la watu kwenye mstari. Wa kwanza kupitia jukwaani alikuwa ni mwanamke Mwislamu, doa jekundu kwenye paji la uso wake, kama mjuavyo Mwislamu shupavu.

Nami nikasema, "Kwa nini ukaja kwangu? Wewe ni Mwislamu."

Akasema, "Ndivyo nilivyo."

Nikasema, "Kwa nini ukaja kwangu, nikiwa Mkristo?"

Akasema, "Kwa sababu nafikiri unaweza kunisaidia." Alizungumza Kiingereza, vizuri sana.

Nami nikasema, "Je, umewahi kusoma Agano Jipya?"

Akasema, "Nimelisoma."

Nami nikasema, "Basi umeona yale ambayo nimemaliza tu kuzungumzia, kwamba Yeye alikuwa nini, yeye yule jana . . . "

Akasema, "Ndiyo, bwana."

24 Nikasema, "Basi kama Roho Mtakatifu atakufunulia, basi utajua ya kwamba nabii wako wa Kiislamu hawezi kufanya hivyo, amekufa na kuzikwa, lakini Kristo, Mwana wa Mungu, amefufuka tena na yu hai milele."

Akasema, "Kama Yeye anaweza kufunua kama alivyofanya, katika Agano Jipya pale, kama linavyosema, nitamkubali kama Mwokozi wangu."

25 Basi wakati . . . nikasema . . . Nikamwanglia tena, nikasema, "Una uvimbe kwenye tumbo la uzazi. Mume wako ameketi moja kwa moja pale nje, yeye ni mtu mrefu mwembamba. Lakini

ulikuwa na daktari siku chache zilizopita, mwenye masharubu meusi, mnene, amevaa suti ya kijivu, naye akakuchunguza ogani ya kike, na kusema, kwenye ovari, una uvimbe."

Akasema, "Ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu binafsi," ndipo Waislamu elfu kumi wakamjia Kristo wakati huo.

26 Kabla sijaenda kule, nilizungumza katika Klabu ya Kiwanis, na wahudumu fulani walikuwepo. Nao walikuwa wakizungumza juu ya mtu mmoja pale, aliyekuwa huko miaka ishirini, na kusema, "Kito hicho cha thamani," alikuwa amembadilisha mmoja kuwa Mwislamu. Halafu wao waliniambia nilikuwa na kichaa, huku kile wanachokiita *kichaa*, na kile wanachokiita *saikolojia* na *telepathia ya kiakili*, ama *pepo mchafu*, ama chochote kile, kiliwabadilisha Waislamu wengi zaidi kwa Kristo kwa muda wa dakika tano kuliko vitini vyote vya kiakili na kila kitu kilichosambazwa katika miaka mia moja na hamsini. Mnaona? Haya basi.

27 Aliyefuata jukwaani alikuwa mvulana mdogo mwenye makengeza. Nikiwa nimemtazama, nilisema, "Sasa, sina uwezo wowote wa kuyanyoosha macho yake, mnajua sina, mimi ni mwanadamu tu. Mwangalieni huyu jamaa mdogo." Kisha nikasema, "Lakini sasa, kuhusu maisha yake . . . " nikimwangalia.

28 Na kwa hiyo basi, nilipokuwa nikizungumza, maskini mvulana huyo . . . Nikasema, "Anatoka katika nyu—nyumba ya Kikristo, kwa sababu katika kibanda chake, unapoingia mlangoni, kuna picha ya Kristo inayoning'inia upande wake wa kulia wa mlango, unapoingia. Mama na baba yake ni Wazulu, lakini yeye ni . . . wao kidogo ni watu wembamba, warefu," nao wakasimama, huko nyuma kabisa, labda bloku moja ya mji huko nyuma, ya kwamba hiyo ilikuwa ni kweli. Nami nikasema, "Sasa, mama, alimwonyesha baba, mara tu macho ya mtoto huyo mchanga yalipofunguliwa, alizaliwa akiwa na makengeza."

29 Nikaangalia nyuma na huyo jamaa mdogo amesimama hapo, tumbo lake dogo limetokeza, hana nguo hata kidogo, naye huyo hapo amesimama pale, akinitazama *hivyo*. Nilipotazama tena macho yake yalikuwa yamenyooka kama yangu, nikasema, "Mtu yeyote anaona macho yake yamenyooka," akapitishwa.

30 Ni wangapi waliowahi kusikia juu ya Dk. F. F. Bosworth, mzee Ndugu Bosworth? Mmoja wa wazee watauwa sana niliowahi kukutana nao maishani mwangu. Huyo hapo, amesimama jukwaani, nikamsikia akijaribu- . . . Ni wangapi waliowahi kumjua Ern Baxter? Mwanatheolojia hodari, ndugu katika Kristo, alikuwa amesimama hapo karibu.

31 Ndipo daktari Mwingereza alikuwa akibishana, akaja pale, na kusema, "Ulimfanyia nini mtoto huyo? Je, ulimpumbaza akili?"

32 Nami nikasema, "Ati nayo serikali ya Uingereza imekupa leseni ya matibabu, huku hujui juu ya kupumbaza akili zaidi ya hapo! Ikiwa kupumbaza akili kutayanyoosha macho ya mtoto mchanga, mwenye makengeza, ninyi madaktari ni afadhali mkapumbaze akili."

33 Kasema, "Vema, Bw. Branham, nilimweka huyu mtoto jukwaani, *pale* chini, nayo macho ya huyu mtoto yalikuwa na makengeza, na *hapa*," alikuwa amesimama hapa, chini ya mkono wake, anasema, "macho yake yamenyooka. Jambo fulani lilitokea kati ya *hapa* na *pale*."

Nami nikasema, "Naam, alikutana na Kristo."

34 Sasa, akasema . . . Yungiyungi kubwa mno . . . Baadhi yenu kina mama mnapenda yungiyungi. Baadhi ya hayo maua ya yungiyungi yana upana wa inchi kumi na nane, na pale, mashada makubwa yake kote jukwaani, Ni . . . akasema, "Ninajua Mungu yuko kwenye ua hilo, nimefundishwa kuamini hivyo, ni uhai. Hatuwezi kulifanya liwepo, hiyo ni kweli, lakini," kasema, "kama . . . je, Yeye yupo hapa vya kutosha kuyanyoosha macho ya huyo mvulana?"

35 Bw. Bosworth akaweka mikono yake juu yake, akasema, "Bwana, utasababisha fujo, angalia huko nje sasa." Kasema, "Unachukua muda mwingi kupita kiasi, wakati huyu Ndugu yuko chini ya upako. Itatulazimu kukuomba uondoke."

Naye akasema, "Hebu kidogo. Bw. Branham, ilikuwaje kwa mvulana huyo? Je, Yesu Kristo yuko hapa vya kutosha kuyanyoosha hayo macho?"

36 Nikasema, "Itakubidi, chukua neno langu, alikuwa amesimama pale *pale*, hata sijamgusa. I—imani ya yule baba na mama, huko nje, pamoja na mtoto huyu, macho yake yamenyooka."

Akasukuma kila mtu nyuma, akaenda jukwaani, akainua mkono wake na kusema, "Basi ninamkubali Kristo kama Mwokozi wangu binafsi."

37 Kisha nilipokuwa nikiondoka, yapata watu elfu ishirini na watano ama thelathini, huko nje kwenye ndege, wakitupungia mikono ya kwaheri, maskini jamaa huyu aliruka juu ya safu zao, zilizokuwa pale, na kukimbia huko nje, akanikumbatia shingoni, na kuanza kunena kwa lugha. Naye akasema, "Nimehama. Sasa, nitakuwa daktari mmishenari kwa wenyeji, kule nyuma, chini ya mpangilio wa Kipentekoste." Loo, jamani.

38 Alasiri hiyo, nikiwa nimesimama pale, kisa kimoja tu zaidi, sitakuwa na wakati wa kukisimulia, lakini hilo lilipotokea, nilisema, "Ni wangapi kati yenu wanaotaka kumpokea Kristo kama Mwokozi binafsi? Nataka uinue mkono wako." Elfu thelathini walisimama, wenyeji wavaao blanketi elfu thelathini,

hawakujua mkono wa kulia wala wa kushoto, wanawake wamesimama pale, bila nguo, kipande tu cha inchi nne, shanga.

Ndipo mtu fulani akasema, "Ninaamini walimaanisha uponyaji wa kimwili."

39 Nikasema, "Sikumaanisha uponyaji wa kimwili. Je, mnasadiki kwamba Biblia, ambapo ndio kwanza niwaambie Yeye alikuwa ni Nani, ni Mungu anayefanya hivi?" Kila mmoja wao akainua mikono yake juu. Nikasema, "Ikiwa wewe ni mwaminifu, ivunjie sanamu yako chini." Ilikuwa kama dhoruba ya mavumbi, namna *hiyo*, nao wenyeji elfu thelathini wavaao blanketi wakampokea Kristo kama Mwokozi wao kwa wakati mmoja.

40 Ndipo kesho yake asubuhi Sidney Smith, meya wa Durban, Afrika Kusini, akanipigia simu na kusema, "Nenda kwenye madirisha yako, yanayoangalia ufuko wa bahari, upesi sana, utaona kitu ambacho hujawahi kuona." Ndipo yakatokea malori kumi na saba ya mizigo, magari makubwa, nayo ni marefu kama kutoka *hapa* hadi pale inaposema "Kutoka" *pale*, yamejaa tu . . .

41 Nilifanya ombi moja, ombi la kusanyiko, kwa hao maelfu mara maelfu, bahari tu za watu, mmeona picha zake. Halafu basi. . .Hayo ni mabadiliko katika jambo hili. Na wakati—wakati unapoangalia kule. . .Nami nikatazama kule nje, nao walikuwa wako huko nje nami nikasimama tu na kuinua mkono wangu, na kufanya ombi moja dogo la kama dakika tano, juu ya kila mmoja wao na kusema, "Kama unaamini ya kwamba Roho huyo, anayejua siri za moyo, ni Mungu wa Biblia, basi ukubali uponyaji wako."

42 Ndipo kesho yake nikachungulia dirishani, na kumi na saba ya malori hayo makubwa yaliyojaa mizigo yanashuka, nao hao wenyeji waliokuwa wakitumia vitu hivyo walivyokuwa wakibebewa, na marungu, na viti vya magurudumu, na machela na chochote kile, walikuwa wakitembea nyuma yake, wakiimba, "Mambo yote yanawezekana, amini tu."

43 Dk. F. F. Bosworth ni mmoja wa watu waaminifu sana niliowahi kuona, hangeweza kamwe. . .angetoa makadirio ya chini badala ya kupitisha makadirio, alisema, "Ndugu Branham, nilipoona jambo hilo kubwa mno likitukia," kasema, "Ningeweza kusema huku mkono wangu ukiwa juu ya Biblia kwamba kwa makadirio ya chini miujiza ya ajabu sana elfu ishirini na tano ilitendeka kwa wakati mmoja."

44 Nasi tunageuza vichwa vyetu, na kuondoka, na kusema, "Vema, nadhani ilikuwa sawa." Watasimama na kutuhukumu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ninyi ni watu wangu, mimi ni Mwanglo-Sakson, ninyi ni—ninyi ni watu wangu. Ninyi ndio ambao mimi . . . Wewe ni—wewe ni kama mimi, wewe ni mzungu, na—na mimi—mimi ni—mimi ni—niko hapa kukwambia, lakini elimu yenu imewaharibu. Hiyo ni kweli kabisa. Imewapeleka

mbali na Mungu, daima hufanya hivyo. Elimu ndiyo adui mkuu sana Injili imewahi kuwa naye, ninasema hivyo kwa moyo wangu wote, ndiyo adui mkubwa sana ambaye Injili imewahi kuwa naye. Ni vigumu zaidi kushughulika na kafiri mwenye elimu kuliko yule ambaye hana elimu.

45 Hebu niwaambie jambo fulani, mahali papo hapo, nami nikawauliza watu hawa, nikasema, "Msingoje sasa hadi mjifunze lugha, nendeni, mkamwambie kila mtu katika kabila lenu." Ninayo mikato ya magazeti ambapo, nasahau ni shehena ngapi za bunduki na kadhalika ambazo walikuwa wameiba, katika kabila la Washangai tu, walizirudisha. Meya wa . . . Gazeti la Durban lilitangaza, kwamba walikuwa wamemalizana na dhambi.

46 Pia angalieni, hebu niseme jambo fulani tu, sio kukufuru, bali kuwa ndugu, na mtauwa, na kwa maonyo kwenu: Hao wanawake, huku wamesimama pale uchi wa mnyama, bila kitu ila kipande kidogo, na mara—mara walipompokea Kristo kama Mwokozi wao, waliondoka pale huku wamekunja mikono yao. Hebu jibu swali langu, mtu fulani: Ikiwa kumpokea tu Kristo kutamfanya mwa—mwanamke, asiyejua mkono wa kulia wala wa kushoto, kutambua kuwa yu uchi, tunawezaje kujiita Wakristo na daima tunaendelea kuvua nguo? Kuna kasoro mahali fulani. Na tuombe.

47 Baba wa Mbinguni, nimejaribu sana, nimefanya yote nijuayo, mengine ni Kwako, Baba. Ni—ninaninii tu . . . Naomba utusaidie sasa tunaposoma Neno Lako, tunapozungumza. Chochote ulichokiita, hakika Wewe . . . kitakuja. Ninayakabidhi yote Kwako, pamoja na mimi mwenyewe, Maneno haya machache ambayo yamewekwa hapa mbele yangu. Nami ninaomba ya kwamba utalitakasa ili kukuadhimisha Wewe.

48 Samahani ninawachelewesha watu Wako sana. Nami naomba, Baba, nikijua ya kwamba uamsho umekwisha, nao watu huchoka kwa urahisi, sa—samahani ikiwa nimefanya kosa lolote. Nami naomba ya kwamba utanisaidia, usiku wa leo, na utujalie tulione Neno Lako, kwa mara nyingine tena, katika Nuru Yake, kisha uwaponye wagonjwa na uwaokoe waliopotea. Tunalikabidhi Kwako katika Jina la Yesu. Amina.

49 Mathayo Mtakatifu 12, kuanzia ninii . . . kwenye kifungu cha 38. Ninyi ni—ninyi ni wazuri sana nachukia tu . . . Nachukia kulazimika kujibana. Mnaona? Nasi tumezoea wakati wa uamsho, tunapohubiri usiku kucha, tunaomba usiku kucha, usiku baada ya usiku, mnaona, wakati wote, tukienda daima. Uamsho unapoanza, ni mchana tu na usiku, mchana na usiku. Sijali mkikosa kwenda kazini kwa siku moja, hiyo ni sawa, lakini siwataki, mkose shule ya Jumapili asubuhi; msi—msikose shule ya Jumapili. Ikiwa itakubidi kukosa kazi ya siku moja, sitajisikia vibaya sana kuhusu hilo, kwa sababu mambo hayo

yote kwa vyovyote vile yanaharibika, ila msikose shule ya Jumapili. Nitawaachilia mapema mpate kuhudhuria shule ya Jumapili.

Kifungu cha 38 cha Mathayo 12:

> Basi kulikuwa *baadhi ya waandishi . . . wa Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.*
>
> *Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa* kinatafuta . . . *ishara; wala hakitapewa ishara, ila ishara ya nabii Yona:*
>
> *Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi; hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.*
>
> Pia *watu wa Ninawi watasimama katika hukumu pamoja na kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.*
>
> *Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.*

50 Ninataka kuchukua somo dogo kutoka hapo: *Tazama, Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa.*

51 Yesu alikuwa . . . Ninaweka saa yangu king'ora, ili nijue sitapitisha muda, usiku wa leo. Yesu alikuwa akiikemea miji ambayo alikuwa ametoka, naye alikuwa amefanya kazi na ishara Zake. Alikuwa akiwakemea kwa sababu hawakumwamini. Kama utasoma mlango uliotangulia, mlango wa 11, na kusoma mlango wa 12 utaona, hapo ndani, ambapo hao watu waliopaswa kuijua siku waliyokuwa wakiishi, hawakuijua, walikosa kuitambua.

52 Na badala ya kujua hasa siku na ishara ambayo ingekuwa katika siku Zake . . . Hata aliwakemea, akasema, "Mnaweza kuutambua uso wa anga; lakini ishara ya wakati hamwezi kuitambua. Kama mngenijua Mimi, mngaliijua siku Yangu."

53 Sasa, hebu tujaribu tu kunywa kila sehemu ya haya, usiku wa leo. Nami najua ni tofauti, masomo haya yamefanyizwa tofauti, mimi . . . na yale labda mmekuwa mkisikiliza, bali nataka mjaribu kusikiliza kwa makini, usiku wa leo. Mnaona, walikuwa—walikuwa wakijaribu ku—kuwa na mawazo yao wenyewe, wala si kumsikiliza Kimaandiko, kwa maana alikuwa amewaambia, "Kwa nini hamyachunguzi Maandiko, kwa kuwa Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi; ndani Yake mnafikiri mna

Uzima wa Milele Nayo yananishuhudia Mimi. Na kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi."

54 Wasingeweza kumwamini kuwa Mungu na hata hivyo ni Mwanadamu. Akasema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, kama Mwanadamu, ziaminini hizo kazi. Acheni kazi zishuhudie, endapo hamwezi kuniamini Mimi. Wakisema nimezaliwa kiharamu, wala sina elimu, sikuwahi kuonekana katika yoyote ya shule zenu, na kadhalika, wala hamwezi kuniamini kwa sababu sijapata kuwa chini ya mafundisho yenu au kadhalika, mbona, aminini kazi nizifanyazo; hizo zinanishuhudia Mimi." Ni karipio jinsi gani kwa wa—wa—watu.

55 Sasa angalieni, miji yote aliyokuwa ameenda, Naye alikuwa akiukemea Kapernaumu, "Umekuzwa mpaka Mbinguni, lakini utashushwa mpaka kuzimu. Kama matendo makuu, yangelifanyika kwako . . . yaliyofanyika kwako, yangalifanyika Sodoma, ungalisimama hata wa leo." Naye akaanza kuzungumzia mmoja kwa mwingine, jinsi ambavyo . . .

56 Kuna mtu fulani mgonjwa *hapo*. Ikiwa baadhi ya ndugu watamtoa nje, na kumchukua, ama, kumwombea. Mwekeleeni tu mikono yenu, Ndugu, na hebu nimwombee, papa hapa.

57 Baba yetu wa Mbinguni, ninamwombea dada huyo. Jalia nguvu za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na kumkomboa, Bwana. Ninaomba haya katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

58 Sasa, jambo ni kwamba, anaumwa sana kwa sababu ya msongamano *hapo*, huku u—umati umemzunguka. Kuna mtu anayeketi *hapa*, papa *hapa*, akinitazama moja kwa moja, anasumbuliwa na kitu kile kile. Kwa hiyo ninii tu . . . Ukitaka kumchukua na kumtembeza huku, au kumtoa nje, na kumwacha apate hewa kidogo na kadhalika, kisha umrudishe, itakuwa sawa.

Sasa, wakati wakifanya hivyo, ninyi sikilizeni yale tu—tunayojaribu kusema hapa. Sasa, angalieni. Huenda ikawabidi kumbeba, kwa sababu amezimia. Unaona?

59 Sasa, angalieni, Yesu alisema ya kwamba alikuwa akiwakemea watu hao kwa sababu kwamba walikuwa ta—tayari wamemkataa, katika mambo aliyokuwa akifanya, wala wasingeweza kuyaelewa. Naye alikuwa anawaambia habari zake. Sasa, Mungu alikuwa akiwarudia, kwa sababu ya kutokuamini kwao.

60 Sasa, tunajua hili, ya kwamba katika kila kizazi, ambacho kimekuwako duniani, Mungu daima ameonyesha karama Zake na ishara na maajabu ya thibitisho la Neno Lake, daima. Na watu, hata katika Agano la Kale, katika siku ambazo Yesu alikuwa akirejea hapa, Yeye . . . Kwa kweli, kwa uaminifu, walitegemea zaidi ishara kuliko walivyotegemea theolojia, kwa sababu kama theolojia, haidhuru ilionekana kuwa kuu jinsi gani, na jinsi ilivyoonekana kuwa sahihi, kama Urimu na Thumimu

hazikusema kwamba ilikuwa sahihi, ilikuwa ni uongo. Mnaona? Walitegemea ishara ya kimbinguni, lakini ishara ya kimbinguni haikuweza kuja juu ya chochote, ilibidi ije kulingana na Neno.

61 Sasa, hivyo ndivyo tunavyopaswa kutazama, siku hizi. Tuna ishara za kila namna, lakini hazina budi kuwa ni ishara kutoka katika ahadi ya Neno, ahadi ya Neno kufanya jambo hili. Nasi tunajua ya kwamba, katika siku hii, tunaweza kutafuta mambo ambayo si ya kweli, hakika tunaweza, kwa sababu Shetani analitupa jeshi lake lote huko nje, kufanya kila awezalo kufanya, kulizuia, lakini kamwe hatalifanya. Neno la Mungu litashinda, litaendelea mbele moja kwa moja. Kwa hiyo hatalizuia kamwe, hilo ni jambo moja la hakika.

62 Sasa, Mungu daima aliwatumia ishara, na kuwaambia waamini manabii wao, na kadhalika, katika Biblia. Halafu Yesu hapa, alipokuwa amesimama pale, baada ya kufanya mambo mengi sana, ndipo hawa hapa Mafarisayo wanakuja na kusema, "Bwana, twataka kuona ishara Kwako," walipokuwa wamemwona akifanya vile hasa Biblia ilisema angefanya, na hata hivyo wakarudi tena, kasema, "Tungetaka kuona ishara kwako."

63 Naye akawaangalia, nawazia kidogo amevunjika moyo na kusema, "Kizazi kibaya na cha zinaa kinatafuta ishara; wala hawatapokea ishara ila ishara ya Yona," maana yake Yona, nabii, "kama alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi; vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi." Sasa, nawatakeni . . . Sasa, angalieni ni kizazi cha namna gani kingetafuta ishara hii: kizazi kibaya, kiovu, kisichoamini, cha zinaa.

64 Ni wangapi wanaojua, na wanatheolojia na wasomaji wa Maandiko wanaojua, ya kwamba sikuzote, Biblia ina jibu maradufu? Daima hujibu na kujibu tena, hujirudia, haiwezi kufa kamwe, ni Neno la Milele la Mungu. Na hapa katika Mathayo m—mlango wa 3, Yeye alisema hapa, Alisema, "'Kutoka Misri ni . . .' Ili litimie lile lililonenwa na nabii, 'Kutoka Misri nimemwita Mwanangu.'" Fuatilia maandishi yako ya pambizoni uone huyo alikuwa ni nani, alikuwa ni Yakobo mwanawe, lakini pia ilimrejelea Kristo, Mwanawe. Sikuzote lina jibu maradufu.

65 Na sasa, Yesu, bila shaka, alikuwa akimaanisha kizazi hicho, lakini kizazi chochote kibaya na kisichoamini, cha zinaa. Na ikiwa hii haitakidhi sifa zake, kizazi hiki tunachoishi siku hizi, ulimwenguni kote, sijui ni kipi kinakidhi. Tunaishi katika wakati wa mojawapo ya vizazi visivyoamini, vya zinaa ambavyo vimewahi kujulikana.

66 Nilichukua gazeti, nilipokuwa nikiruka juu ya Hollywood, hapa si muda mrefu uliopita, ama, Los Angeles, nami nilikuwa nikisoma ambapo kwamba uhalifu mkubwa sabini na nne

ulitendwa kila usiku, uhalifu mkubwa, katika mji mmoja: Los Angeles. Nilikuwa nikisoma kwenye gazeti la Chicago, si muda mrefu uliopita, ambapo tatu. . . visa elfu ishirini na tano vya utoaji mimba vilitambuliwa katika jiji la Chicago kila mwezi, wazieni hilo, na ambapo ushoga katika Pwani hii ya Magharibi ulikuwa umeongezeka kwa asilimia thelathini tangu mwaka jana. Wazieni hilo, "Kizazi cha zinaa!"

67 Loo, laiti tungekuwa tu na hadi yapata saa nane usiku kulichimbua hilo: uovu, kizazi cha zinaa. Kingekuwa cha aina hiyo, nao wangeipata. Ilikuwa ni nini? Ishara ya ufufuo. Sasa, tuko wapi?

68 "Kama vile Yona alivyokuwa ndani ya tumbo la nyangumi, Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi." Watu wengi, siku hizi, wanafikiri kwamba bado yuko huko, lakini Yeye hajafa, amefufuka katika wafu na yuko hapa pamoja nasi sasa, akionekana miongoni mwetu, akijithibitisha Mwenyewe, juu na chini pwani, kote ulimwenguni kila mahali, kwamba Yu hai. Nacho kizazi kiovu na cha zinaa kinaona ishara kwamba Yesu Kristo yu hai wala hajafa. "Kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara," nao wataipata, ishara ya ufufuo. Hebu likolee ndani sana sasa; someni kwa bidii.

69 Wakati mkiacha hilo likolee nataka kuwaulizeni jambo fulani kuhusu Yona. Yona alikuwa nabii. Watu wengi wanamhukumu Yona na kusema, "Vema, alikuwa maskini mtu aliyerudi nyuma. Yeye. . . " Hakuwa amerudi nyuma. Mtu wa Mungu, "Hatua. . . hatua za wenye haki huongozwa na Bwana." Je, unaamini hivyo? Wala sijali yale mtu wa Mungu afanyayo, kama ameteuliwa na Mungu, anaweza kufanya mambo ambayo anadhani ni kichaa kwake mwenyewe, lakini kama utaangalia tu, inatenda kazi sawasawa kabisa, kama ataenda tu jinsi anavyoongozwa.

70 Sasa, Mungu alimwambia Yona ashuke kwenda Ninawi, jiji lenye ukubwa wa St. Louis. Waovu? Loo, jamani! Na wapotovu, wamepotoka, kila kitu kilikuwa kibaya kwao. Alisema, "Shuka uende huko na kulia dhidi yao." Naye akashuka kwenye meli na kujinunulia tiketi. Badala ya kwenda Ninawi, labda hakuna merikebu yoyote iliyokuwa ikipita njia hiyo, kwa hiyo akaenda tu Tarshishi. Siamini ya kwamba ilikuwa ni ujinga, baada ya mimi kupata ufunuo wake halisi, na kuona kilichotukia, na kusoma Vitabu juu yake, nami ninaona ambapo alikuwa sahihi.

71 Basi akienda zake baharini aliingia katika matatizo. Ndipo dhoruba zikatokea, nao wakafikiri hiyo meli ilikuwa inaenda kuzama. Basi Yona akawaambia kuwa ni kosa lake, wamfunge mikono na miguu na kumtupa baharini. Naye Mungu alikuwa ametayarisha nyangumi kummeza.

72 Sasa, miaka kadhaa iliyopita, kama miaka ishirini na mitano iliyopita, walileta u—umbo la nyangumi huko Louisville,

Kentucky; huko ni ng'ambo tu ya mto kutoka ninapoishi. Nao walionyesha ukubwa wa kinywa chake, ndipo maskini profesa fulani, akisimama pale, ambaye alikuwa na elimu nyingi kuliko vile alivyokuwa na busara ya kuidhibiti. Kwa hiyo alikuwa akielezea yote kuhusu nyangumi huyu.

73 Naye akasema, "Sasa, mmesikia ile hekaya ya kale kuhusu nyangumi kummeza Yona." Akasema, "Kama ukiangalia, usingeweza kutia besiboli kooni mwake." Kasema, "Si kitu kama hicho."

74 Aah! Nilikuwa tu Mwairishi kupita kiasi kuvumilia hilo. Kwa hiyo nikasema, "Ningependa tu kukwambia jambo fulani, jamani. Kuna jambo moja ulilokosa, huenda nyangumi *huyo* asiweze kuumeza, lakini kama ukiangalia, Mungu alimtayarisha *huyu*. Huyo alikuwa wa aina maalum, ungeweza kurusha mashua nzima kwenye koo lake, labda." Mnaona? Mungu alimwandalia Yona samaki, mnaona, alikuwa ameundwa kimaalum, aliundwa kulingana na maagizo, apate kummeza nabii. Naye. . .Na ilikuwa. . ."Hakuna kitu kama hicho. . ." Watu. . .

75 Kidogo. . .Sio mahali pa kutania, lakini ni—nilikuwa. . . Msichana mdogo alikuwa ameokoka, naye alikuwa akipanda barabarani akipiga mayowe, "Bwana asifiwe," na kuimba, maskini nywele zake zimelazwa nyuma, nao uso wake uking'aa kama kitunguu kilichomenywa, alikuwa na wakati mtukufu.

Kafiri mmoja alikuwa amesimama pembeni, kasema: "Kwani kuna nini?"

Kasema, "Niliokolewa, *kule* chini, muda mfupi uliopita. Bwana asifiwe."

Kasema, "Una nini juu ya moyo wako?"

Kasema, "Biblia."

Kasema, "Nadhani unaiamini."

Kasema, "Hakika, ninaiamini."

Kasema, "Unaamini hadithi hiyo hapo ndani kuhusu Yona?"

Kasema, "Hakika, ninaiamini hadithi hiyo kuhusu Yona."

Akasema, "Unaamini kwamba—kwamba Yona alimezwa na nyangumi?"

Akasema, "Loo, naam. Kama Biblia ilisema—ilisema kwamba Yona alimmeza huyo nyangumi, ningeiamini." Ndipo akasema. . .

"Loo," kasema, "utathibitishaje jambo hilo kwa njia nyingine ila kwa imani?"

"Mbona," akasema, "nitakapofika Mbinguni nitaenda tu na kuzungumza na Yona kuhusu jambo hilo."

Kasema, "Basi itakuwaje kama Yona hayuko huko?"

Kasema, "Basi itakubidi wewe kumwuliza." Nadhani hiyo ilitosha. Naam. Kwa hivyo huyo mtoto mchanga . . . Lakini hata hivyo Mungu anaweza.

76 Basi Yona akatupwa nje ya meli, naye huyo nyangumi, akizunguka-zunguka majini akiwinda chakula chake, akammeza Yona. Na mtu yeyote anajua, kama vile kuwalisha samaki wako wa dhahabu, huyo samaki mdogo anapokula nalo tumbo lake linashiba, yeye hushuka moja kwa moja chini ya mtungi, ambamo umemweka ndani, kile chombo kidogo, naye analaza pezi zake ndogo chini, amekula, anapumzika. Basi samaki huyu, alipommeza mhubiri huyu, akashuka chini ya bahari kupumzika. Sijui alishuka chini mita ngapi, lakini alikuwa amelala mle chini.

77 Nami ningependa kuzungumza juu ya hili sasa. Unajua u—unakuta watu wengi wanaotegemea dalili, "Vema, niliombewa, nina mkono uliolemaa, niliombewa, lakini, kwe—kweli ninamwamini Mungu, lakini mkono wangu haujapata nafuu." Hautawahi kupata nafuu maadamu unautazama mkono huo. Unaona, unaangalia kwingine, huna budi kuangalia ahadi Yake.

78 Wakati fulani uliopita, maskini mume na mke, wakongwe, walikuja wakitaka niende nikamwombee mvulana wao, alikuwa yuafa kwa dondakoo jeusi. Nami sikuninii . . . nisingeweza kwenda. Nami nikaendelea kungoja, ndipo siku chache baadaye yule mzee akasema, "Mvulana wangu sasa yuafa." Basi hatimaye, baada ya ibada nikaenda.

79 Daktari asingeniruhusu kuingia, naye akasema, "Hasha, una watoto, wala siwezi kukuruhusu uingie kwa sababu dondakoo hiyo inaambukiza." Kisha akasema, "Usingeweza kumsaidia kwa vyovyote."

80 Nami, nikizungumza na huyo mtu, nikagundua kwamba alikuwa Mkatoliki. Ndipo nikasema, "Ikiwa kasisi alikuwa hapa . . . Kama—Kama mvulana huyo alikuwa Mkatoliki, na—naye baba huyu alikuwa amekuja akanichukua, nami nilikuwa kasisi . . . "

Akasema, "Hiyo ni tofauti," akasema, "unaona, kasisi hajaoa."

Nikasema, "Ungemruhusu aingie achukue . . . amfanyie taratibu za ibada za mwisho, sivyo?"

Akasema, "Naam, lakini kasisi si mtu aliyeoa, wewe una watoto."

81 Nikasema, "Vipi nikijichukulia hilo jukumu mwenyewe? Nitasaini karatasi, nijitwike hilo jukumu." Hatimaye, nikamshawishi, akanivalisha kama Ku Klux Klan, na vitu vya kila namna juu yangu, kisha akanituma kule alipokuwa mvulana huyu.

82 Sasa, uliingia moyoni, shida fulani moyoni mwake. Kadiogramu ilionyesha kuwa ulikuwa umeingia ndani sana, na ukipiga tu mara *kadhaa* kwa dakika. Ndipo maskini mama na baba wakasimama pale, kando ya huyo mvulana, nikaenda kando ya kitanda nao upande mwingine, naye maskini nesi mmoja akasimama pale akitutazama, msichana mwenye sura nzuri wa karibu, loo, nadhani, umri wa miaka ishirini na mitano. Na kwa hiyo nikaweka mikono yangu juu ya mvulana huyo, na kuomba, na kuomba tu maombi ya kawaida.

83 Ndipo niliposema, "Amina," maskini huyo baba akamshika mama na kuanza kumkumbatia, naye...wakakumbatiana. Wakasema, "Loo, Mama, si ni ajabu hiyo? Si ni ajabu hiyo? Asante, Bwana Yesu, kwa kumponya mvulana wetu."

84 Mvulana huyo alikuwa mahututi tu alivyowahi kuwa, nao wakafutiana tu machozi kutoka machoni mwao na kumsifu Mungu. Ndipo maskini nesi huyo, akisimama pale, asingeweza kuelewa hilo, naye akasema, "Bwana, ni sawa, nadhani," kasema, "Mimi si wa dini yenu, lakini...aina yenu ya dini," akasema, "lakini nataka kuwaulizeni jambo fulani. Mnawezaje kutenda hivyo, wewe, na mama wa mtoto huyu kutenda hivyo, huku mvulana huyo amelala hapo akifa?"

Akasema, "Bibie, huyu mvulana hafi."

"Mbona," akasema, "amezimia siku tatu."

85 Na aina fulani ya mtambo pale ilionyesha kwamba hii ikipata kushuka *hivyo*, kamwe, katika historia ya matibabu, haijawahi kurudi tena. Maskini huyo baba, sitalisahau kamwe, akayapangusa macho yake, akaenda pale, kisha akaweka mikono yake juu ya bega la msichana huyo, akasema, "Ewe mtoto," akasema, "umefundishwa kuuangalia huo mtambo, hayo tu ndiyo unayojua juu yake, ni 'Angalia mtambo huo.'" Kasema, "Hivyo—hivyo...Yote mtambo huo ujuayo ni yale yanayoendelea *hapa*. Hiyo ni kweli." Kasema, "Unauangalia mtambo huo, lakini ninaiangalia ahadi ambayo Mungu alitoa."

86 Inategemea kile unachoangalia. Mvulana huyo ameoa na ana watoto wawili. Mnaona, inaonyesha tu. Mnaona? Alikaa namna hiyo siku zingine mbili ama tatu, lakini alitoka moja kwa moja na akapona. Mnaona, inaonyesha tu kile unachoangalia. Huna budi kuona kile unachoangalia. Usiangalie dalili zako.

87 Kama mtu yeyote alikuwa na dalili, Yona alikuwa nazo. Sasa, kumbukeni, alikuwa katika tumbo la nyangumi. Tuseme alikuwa katika kina kirefu cha mita ishirini kule nje baharini, huku mikono yake imefungwa nyuma yake, miguu yake imefungwa, na katika tumbo la nyangumi, amelalia matapiko ya nyangumi tumboni mwake, amezungushiwa mwani kote shingoni mwake. Sasa, hizo kweli ni dalili. Angeangalia *huku*, lilikuwa ni tumbo la nyangumi, *huko* kulikuwa ni tumbo la nyangumi, kila alikoangalia kulikuwa ni tumbo la nyangumi. Sasa, hizo ni dalili

kwelikweli. Hakuna hata mmoja wenu aliye katika hali mbaya hivyo usiku wa leo, nina hakika, hiyo ni kweli, si mbaya hivyo. Kila mahali alikoangalia kulikuwa ni tumbo la nyangumi.

88 Lakini mnajua alichosema? "Ni ubatili wa uongo, sitaziamini." Alisema nini? "Mara nyingine tena nitalitazama hekalu Lako takatifu," akalala chali, akageuka, vizuri sana alivyoweza, kuelekea hekaluni.

89 Kwa nini? Sulemani alipoweka wakfu hekalu hilo, aliomba dua siku hiyo, wakati ile Nguzo ya Moto ilipoingia na kushuka nyuma ya Patakatifu pa patakatifu, Sulemani aliomba, na kusema, "Bwana, ikiwa watu Wako wana shida popote, na kutazama kuelekea mahali hapa patakatifu, basi sikia kutoka Mbinguni," naye akaamini.

90 Naye Mungu akafanya jambo fulani, sijui alilofanya. Huenda aliweka tangi la oksijeni kwenye tumbo la nyangumi huyo, sijui alilofanya. Akamdumisha hai siku tatu mchana na usiku, akampeleka safarini mwake, alikopaswa kwenda.

91 Na kama Yona, chini ya mazingira hayo, angeweza kuamini katika maombi ambayo yalifanywa na mtu ambaye hatimaye alirudi nyuma, kwa sababu ya wanawake, kama Sulemani, na akaamini hekalu lililojengwa kwa mikono ya wanadamu, ni zaidi sana vipi sisi, usiku wa leo, tunapaswa kumwangalia Kristo, ambaye ameketi mkono wa kuume wa Mungu, na Damu Yake Mwenyewe ikifanya maombezi tunapoungama! Jinsi tunavyopaswa kuliamini! "Hakuna kitu, hakuna dalili, itakayosimama njiani, ninaangaia ahadi ya Mungu aliyosema kwamba Yeye angefanya." Hilo ndilo jambo pekee, iangalie hiyo. Huyo hapo.

92 Nilisoma hadithi juu yake wakati mmoja, watu wote wa Ninawi walikuwa makafiri. Makafiri kwa kawaida huabudu wanyama na uhai. Huko chini kabisa Marekani Kusini, niliwaona wakicheza ngoma ya kangaruu. Walikuwa na dansi, aina fulani ya karamu, na wote wakacheza kama tu kangaruu, kwa sababu hicho ndicho chote walichopata kuona, kangaruu tu. Kwa hiyo walikuwa wakitaka kumla huyo kangaruu moja kwa moja, nao wakamtupa motoni na kumwunguza kidogo. Na, loo, jinsi walivyofanya jambo hilo, sijui, sikuwa na njaa. Kwa hiyo basi, kwa vyovyote vile, wao. . . jinsi walivyokuwa wakicheza kama tu ngoma ya kangaruu. Hivyo ndivyo wao . . .

93 Nanyi mnawaona wakija kote Afrika, wana kila namna ya vitu vidogo vya ajabuajabu vya wanyama, vilivyonyunyiziwa damu. Vema, hivyo ndivyo wanaamini kuwa ni Mungu.

94 Na sasa, tunaona ya kwamba watu hawa, kule Ninawi, pia waliabudu sanamu, naye mungu wao wa baharini alikuwa nyangumi. Kwa hiyo watu wote, kazi yao ikiwa ni kando ya bahari, walikuwa wavuvi, kazi kuu. Nayo ilikuwa biashara ya nje kubwa sana huko ya samaki kwa ulimwengu wakati huo.

95 Hivyo basi, ninii . . . wavuvi wote walikuwa huko nje yapata adhuhuri siku moja, wakivua samaki, wakivuta nyavu zao. Na mara ghafla mungu akapanda kutoka baharini, mungu-nyangumi, akaenda mbio ufukoni, na kuutoa ulimi wake, naye huyo nabii akaja akitembea moja kwa moja juu ya huo ulimi wa nyangumi, moja kwa moja hadi ardhini. Si ajabu walitubu. Amina.

96 Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo. Hata hivyo, katika urahisi wake Mungu anajua jinsi ya kulifanya. Mnaona? Yona hakuwa amerudi nyuma, alikuwa tu anafuata uongozi wa Roho, hiyo ndiyo njia ya kuwafanya watu watubu. Yeye . . . Naye akashuka moja kwa moja kupitia mjini, akasema, "Msipotubu, katika siku arobaini mahali hapa patazama." Hivyo tu. Mnaona, wangewezaje kufanya lolote ila kutubu? Kwa sababu mungu wao mwenyewe alimtapika huyo nabii. Walijua alikuwa na Ujumbe. Huyo alikuwa ni mungu wao, hivyo wao . . . Alimtapika tu moja kwa moja.

97 Mungu wetu ni Kristo, amina, Naye alimshusha Roho Mtakatifu. Kwa nini hatuwezi kumwamini? Nini, nashangaa. Hapa Yeye alidhihirishwa katika mwili, hapo alisimama, Naye akasema, "Nao watu wa Ninawi watasimama siku ya mwisho pamoja na kizazi hiki, na kuwahukumu kuwa wamekosa, kwa sababu walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona." Basi mwombeni Ishara!

98 Ndipo anaendelea kusema, yapata wakati huo, kwamba Mungu . . . Kupitia vizazi vyote, jamani, wakati wowote Mungu anapotuma karama duniani, nao watu wanaipokea, huo ni wakati wa ufanisi kwa kizazi hicho, lakini wanapoikataa, ni machafuko kwa kizazi hicho.

99 Sasa, vipi kama, usiku wa leo, iwapo Wamarekani, wanaodai kuwa taifa la Kikristo, vipi kama sisi sote, tunaodai kuwa Wakristo, tungeikubali Karama ya Mungu ambayo Yeye alituma kwetu, Roho Mtakatifu? Si ingekuwa ni ajabu? Mbona, tungeweza kuacha kutengeneza makombora. Mbona, kamwe kusingekuwako na kitu chochote ulimwenguni cha kutudhuru. Wasingeweza, tuna ulinzi, Roho Mtakatifu yuko juu yetu. Hakika. Tusingehitaji kitu kingine ila Roho Mtakatifu, kama watu wangekubali tu Karama ambayo Mungu aliwatumia, na hiyo ni Roho Mtakatifu.

100 Lakini kanisa moja litatofautiana na lingine, na *hili* liseme, "Loo, hakuna kitu kama Roho Mtakatifu, huyo alikuwa kwa ajili ya wale wanafunzi." Naye Ndiye Karama sasa hivi, ni kwa ajili ya Kanisa, na sasa katika siku za mwisho.

101 Mbona, si lazima uzungumze juu ya makimbilio ya mabomu. Watu wanajichimbia chini ya ardhi kama fuko, wakijaribu kulitoroka bomu la atomiki. Utafanyaje hilo? Mbona, watalipua shimo ardhini yapata kina cha maili moja na kwa maili mia

moja na hamsini mraba. Vema, kama ulikuwa maili hamsini chini ya ardhi, moja kwa moja chini ya la—lava, mtikiso wake ungevunja kila mfupa mwilini mwako. Hakuna njia hata kidogo ya kuepukia, njia pekee, lakini tuna kimbilio la bomu, halijatengenezwa kwa chuma, bali limetengenezwa kwa manyoya, chini ya mbawa Zake tunapumzika. Amina. Na sio *huku* chini, liko *huko* juu. Unapaa juu yake, unapoelea katika . . . paa kifuani Mwake. Hakika. Hilo ndilo kimbilio.

102 Acha niingize hili ndani. Natumaini saa yangu haitalia haraka sana. Lakini angalieni, sikilizeni, enyi watu, siku hizi, wanaogopa sana ukomunisti. Jioneni aibu. Kweli, kwa nini mnaogopa ukomunisti? Ninataka mwanatheolojia yeyote, mwanazuoni yeyote wa Biblia anionyeshe mahali ambapo ukomunisti utautawala ulimwengu. Nawaambia, Urumi utautawala ulimwengu, kulingana na Biblia.

103 Usiangalie hilo. Msiangalie mapazia ya chuma na mapazia ya mianzi, lakini angalieni lile pazia la zambarau, hilo ndilo litakalowashika. Kamwe usiyajali hayo. Hilo . . . Ninyi zingatieni hilo tu, na kusema, "Ndugu Branham alisema hivyo," nawe uliweke katika Biblia yako, uone kama ni kweli.

104 Ukomunisti si kitu ila ni chombo mkononi mwa Mungu, kikifanya kazi moja kwa moja. Mbona, hautakuwa chochote. Hiyo ni kweli kabisa. Usiogope hilo, hilo ni jambo ambalo litakuondoa kwenye mkondo wenyewe wa kutazama. Lakini wasomaji wa Biblia, na watu wanaompenda Mungu, wanadumu na yale ambayo Biblia ilisema. Bila shaka. Angalieni tu hilo.

105 Sasa, hatutaipokea Karama ya Mungu katika taifa hili, kizazi hiki, wameikataa. Watu wanaoiamini wanaitwa walokole, wendawazimu, watakatifu wanaojibingirisha, na chochote kile, wanadharauliwa na kukataliwa, yale tu Maandiko yalisema wangefanya, "Wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wenye kudharau walio wema; wakiwa na mfano wa utauwa, huku wakikana nguvu zake." Ndivyo hasa Roho Mtakatifu alivyosema ingetukia katika siku za mwisho, nasi tuko hapa, enyi marafiki, tuko papa hapa.

106 Maandiko mengine mengi tungeweza kuyaambatanisha nalo, hebu na tuliendelee jambo lingine, yale Yesu aliyosema hapa. Na kama ilivyokuwa katika siku za . . . Katika siku za Sulemani, Mungu alituma karama miongoni mwa watu Wake. Na kulikuwa na wakati mmoja walipoikubali, walimkubali Sulemani, karama ya upambanuzi. Na wakati upambanuzi ulipokuwa juu ya Sulemani, kila mtu alikuwa na moyo mmoja na nia moja. Kila . . . Mbona, kila taifa liliogopa. Hawakuwa na vita. Ha—hawakuwa na vita vyovyote kwa sababu waliwaogopa Israeli, sio sana taifa, bali ni Mungu waliyekuwa wakimtumikia. Walikuwa katika moyo mmoja na nia moja, nao

wote wakakusanyika karibu na karama hiyo. Loo, jinsi wote walivyoipenda, na kila mtu akiongea mema . . .

107 Je, si lingekuwa ni jambo jema kama kila Mkristo, usiku wa leo, Mmarekani, wote wangeanza kuzungumza juu ya Roho Mtakatifu, na jinsi lilivyo jambo zuri, na tu-. . .? Mbona, nawaambia ingekuwa . . . Mbona, hivi si lingeyafanya magazeti kila mahali? Nayo mawasiliano yangeshika moto kutokana na kueneza habari. Loo, ingekuwa ajabu jinsi gani! Lakini hawatafanya hivyo. Mnaona? Lakini loo, laiti tungekusanyika tu kwenye karama za Mungu, Roho Mtakatifu!

108 Sasa, tunaona ya kwamba kila mtu, katika siku hiyo, alijiunga nayo. Naye Mungu akamfanya mtu huyu, ambaye alikuwa na karama hii juu yake, mfalme. Mbona, mnajua, habari zilienea kila mahali, watu wakaleta makundi ya kondoo, wakaleta ng'ombe, na dhahabu, na kila kitu, na kuwasaidia. Walikuwa wakijaribu kupata amani nao, ndivyo walivyokuwa wakijaribu kufanya, kwa sababu walijua ya kwamba Mungu aliye hai alikuwa pamoja na watu walio hai, nao walijua jambo hilo.

109 Sasa, angalieni kilichotukia. Habari zilienea, siku hizo, Mungu ashukuriwe, hawakuwa na televisheni, lakini walikuwa na *mdomo-kwa-sikio*. Nayo mi—misafara ingepitia huko na kwenda mahali fulani, nao wangezungumza habari zake. Ndipo baada ya kitambo kidogo habari zikashuka hadi Sheba. Weka alama kwenye ramani yako ni umbali gani kutoka Yerusalemu hadi Sheba.

110 Walikuwa na malkia huko chini, maskini malkia kafiri, mpagani. Nao watu walikuja na kutoa ushuhuda wa kile kilichokuwa kikiendelea huko Palestina. Na, "Imani chanzo chake ni kusikia Neno la Mungu."

111 Loo, maskini mama huyu alikusudiwa Uzima wa Milele. Na mara aliposikia hili, kitu fulani kikashika moto katika maskini moyo wake wa kipagani, akaanza kushangaa juu ya hilo. Msafara mwingine ulipopita, ilikuwa vigumu kwake kungoja, angewaamuru matowashi wake waondoke waende, kisha anawaita, na kuwaingiza ndani.

"Mlipitia njia gani?"

"Tumetokea kaskazini."

"Je, mlipitia Palestina?"

"Naam. Loo, najua kile unachotaka kuniuliza, kuhusu Mungu wao."

"Naam, hiyo ni kweli. Je, mliiona?"

112 "Niliiona, ni ya kweli. Mbona, wanampenda mtu huyo vizuri sana, walimfanya kuwa mfalme. Naye Mungu wao, wana Mungu wa kimbinguni ambaye anajidhihirisha Mwenyewe moja kwa moja kupitia kwa mtu huyo."

113 Sasa, mtu yeyote anajua...Nitakizima hiki, kwa dakika moja, wakati tu kweli—kweli. Ni...Ni sawa? Dakika moja tu? Uh-huh. Mtu yeyote anajua kwamba ibada ya kikafiri ni, kafiri huleta sanamu, kuhani anamletea divai, anakula kwa sanamu hii, kisha anatoka anaenda hekaluni, anasujudu mbele ya sanamu hii, anaendelea kujichochea namna hiyo, mpaka kweli anaamini kwamba anaweza kusikia sanamu hiyo ikizungumza naye. Sasa, hiyo kabisa ni ibada ya kipagani. Ninyi ndugu mnajua hilo kwa kusoma historia.

114 Sasa, angalieni jinsi Mungu afanyavyo. Anageuka moja kwa moja, wala haninii...Mnaona, wanafikiri ya kwamba u—uhai, roho, ambayo inapaswa kuwa, ambayo kweli ni ya sanamu hiyo, huingia katika sanamu hiyo na kuongea nao. Mbona, ilisemekana kwamba wapagani, zamani za kale, wangeweza kusujudu hivi kwamba, wanadai wangeweza kusikia miungu ikizungumza kutoka kwenye sanamu hizo.

115 Lakini angalieni jinsi Ukristo ulivyo tofauti, jinsi huo ulivyo dhihaka kwake? Mungu hachukui sanamu, Yeye huchukua mtu. Na kama mtu atasujudu katika Uwepo wa Mungu, Mungu hujiingiza Mwenyewe ndani ya mtu huyo, ndipo huyo mtu anakuwa kiumbe hai ambacho Mungu anaishi ndani yake, si sanamu iliyokufa, bali mwanadamu.

116 Mungu hakuwahi kutumia sanamu, daima alimtumia mwanadamu. Mungu hatumii mitambo, vifaa vya kimitambo. Ni...Anatumia mwanadamu, watu binafsi. Samahani, sikukusudia kupiga mayowe kwa sauti hivyo. Angalieni, sijasisimkwa hata hivyo, najua mahali nilipo hasa. Hiyo ni kweli. Najisikia vizuri tu.

117 Angalieni, basi Mungu huyu alikuwa ameshuka, Yehova mkuu, naye akajidhihirisha Mwenyewe kupitia kwa mwanadamu, hata walijua ilikuwa ni zaidi ya mwanadamu, kulikuwa na kitu fulani juu yake ambacho kilikuwa—kilikuwa ni tofauti. Na watu wote walimwabudu Mungu, na kumwamini Mungu, nao wakajenga hekalu, walifanya mambo makuu katika siku hiyo.

118 Angalieni, maskini malkia huyu alipoanza kusikia habari zake, "Imani huja kwa kusikia." Maskini moyo wake ukaanza kudunda kwa kasi, hana budi kupanda kwenda kuiona. Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo walipita watu wengi sana wakishuhudia, kila mtu akielezea jinsi watu hao walivyokuwa na moyo mmoja na nia moja, hakukuwako na tofauti ndani yao, hakukuwako na mtu anayetembea na kusema, "Aa, yeye si wa langu, yeye—yeye ni Farisayo. Sidhani...Mimi ni Msadukayo." Hakuna kitu kama hicho, walikuwa moyo mmoja na nia moja. Hivyo ndivyo hamna budi kuwa.

119 Loo, laiti makanisa yetu yangeweza tu kuwa hivyo, ndugu! Kama makanisa yetu, tofauti zetu, zingeweza tu kuwa...

Vema, ni sawa maadamu mnaamini, na mnaye Mungu, na mnayo makanisa ye—yenu, na kadhalika, lakini loo, hebu tuwe na nia moja, mtu mmoja, *Twendeni Askari Wakristo* mmoja, kitengo kimoja tu cha Mungu kikiendelea hadi kwenye ushindi, kikipokea yote yajayo kwa Jina la Bwana, hilo ni Neno la Bwana aliloahidi kututumia. Liaminini, liwekeni katika matendo.

120 Sasa, jambo la kwanza mwajua, moyo wake mdogo ukaanza kudunda hata asingeweza kukaa tu . . . asingeweza kulala usiku. Ilibidi tu aende akaione.

121 Kuna *jambo fulani* kuhusu unaposikia kuhusu Mungu. Mwanadamu anajua kwamba alitoka kwenye lile pazia la giza, mahali fulani mbali kupita hapa. Wanajua kwamba akifa, anarudi kupitia kwenye pazia hilo. Alitoka wapi na alienda wapi? Mwanadamu sikuzote ametamani kuona kile kilichoko nyuma ya pazia hilo. Kweli kabisa. Basi anapoona kitu kikiinuka kutoka nyuma ya pazia hilo, na kuonyesha jambo ambalo limeahidiwa kutoka huko, linapaswa kuuchangamsha moyo wake.

122 Angalieni, kwa hiyo maskini mwanamke huyu, alikuwa . . . moyo wake ukaanza kudunda aondoke aende. Sasa, alikuwa na mambo ya kufanya kabla hajaenda. Sasa, jambo la kwanza alilopaswa kufanya lilikuwa ni kwenda kupata kibali kutoka kwa kanisa lake aondoke apande kule. Sasa, hilo lilikuwa jambo gumu kumwendea kasisi mpagani. Ninaweza kumwona, wakati yeye . . . akapanda juu, na—naye akainama mbele yake, akamwita, chochote alichofanya, "Baba Mtakatifu," ama chochote kile, akamwendea, akainama, naye kuhani akainama. Naye . . . alikuwa ndiye malkia wa nchi hiyo.

123 Akasema, "Ninasikia, kupitia misafara na kadhalika, na baadhi yao wameniletea Magombo kutoka huko juu Palestina, kwamba wana mkutano mkuu huko. Na kuna mtu huko juu ambaye amepakwa mafuta na Mungu wao, na Mungu huyo anatekeleza Uzima Wake Mwenyewe kupitia mtu huyo. Bwana, Ewe Mtakatifu, ningependa kwenda nikaone."

124 Je, ungeweza kumwazia akimpa ruhusa? "Hatushirikiani na mkutano huo huko juu." Loo, hakika, maneno ya kila namna yangeweza kutokea. "Sasa, kama kuna jambo lolote lingalifanyika, lingalifanyika papa hapa, katika kanisa lako mwenyewe. Na hata hivyo, hilo ni lundo la upuuzi. Tuliwasikia wakivuka bahari na kadhalika namna hiyo, bali ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha, ama," samahani, "walokole, ama chochote kile, mnajua, huko juu. Wao . . . Hakuna kitu hapo. Usiliamini, ni bure. Kama kuna jambo lolote litakalofanyika, litafanyika papa hapa, miongoni mwa kanisa lako mwenyewe. Itakuwa ni papa hapa. Ikiwa kuna lolote—lolote ambalo mungu angefanya, mungu wetu angelifanya."

125 Ningeweza kumwona maskini malkia huyo akijiinua nyuma, akasema, "Bwana, lakini nataka kwenda, nataka kushawishika." Ninapenda ujasiri wa aina hiyo. "Nataka kusadikishwa. Nina Magombo yao hapa, ninataka kwenda kuona kama Roho huyo, aliye ndani ya mtu huyo, yuko vile hasa Magombo haya yanasema kwamba ndivyo Mungu huyo alivyo. Kwa hiyo basi, kama ndivyo, Huyo ndiye Mungu yule anayenena kupitia kwa huyo mtu."

"Sasa, angalia hapa! Huyu hapa mungu mkuu Dagoni, huyu hapa mungu mkuu *Nanii*, Jupita, mungu jua, na hii mingine yote tuliyo nayo hapa."

126 Akasema, "Naam, nyanya wa nyanya yangu aliwatumikia, nyanya yangu akawatumikia na kadhalika, mama yangu aliwatumikia. Na wamefanya nini? Wao ni sanamu bubu, sijawahi kuwasikia wakisema neno au kufanya jambo moja."

127 Ni karibu kama baadhi ya kanuni hizi bubu za imani ambazo tunatumikia siku hizi, na kadhalika, na vitu ambavyo havina uhai zaidi...Wanazungumza juu ya Mungu, Mungu aliyekuwako, na kumpeleka mvulana shuleni, na kumfundisha kuwa mhudumu, na kumwambia kuhusu Mungu wa kihistoria. Je, Mungu wa kihistoria wa jana ana faida gani ikiwa Yeye si Mungu yule yule leo? Ikiwa Mungu aliyejaa rehema angeweza kukidhi mahitaji ya watu jana, kama Yeye si Mungu yule yule leo, Yeye ni Mungu duni, alikuwa na upendeleo.

128 Ina faida gani kumlisha kurumbizi wako vitamini za kila namna kutengeneza mbawa nzuri zenye nguvu na mifupa mikubwa mizito, kisha kumweka kwenye kizimba asiweze kuruka? Ni jambo lile lile kama vile kumpeleka mtu, na kuchukua shule za kila namna, na kila kitu, na kujifunza kile Mungu mmoja alichokuwa, na yote aliyofanya, na yale yote aliyofanya kule, lakini basi kugeuka na kumwambia, "Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama hicho." Hilo hata si la kiakili kwangu.

129 Kwa hivyo huenda maskini malkia huyo alisema, "Nimesikia juu ya miungu hiyo yote, nimesikia juu ya mambo hayo yote, lakini sijawahi kuona msogeo wa uhai kutoka kwao. Sijapata kuona jambo moja likifanywa kutenda kama mungu ama kitu kingine chochote."

"Vema sasa, hebu nikwambie jambo fulani, binti yangu. Kama ukienda huko juu...Wewe ni malkia wetu, huwezi kwenda miongoni mwa kundi la watu kama hao, wapumbavu."

130 Afadhali niseme, linanichoma hata hivyo. Nilikuwa... Binti-mkwe wangu na mke wangu walikuwa katikati ya mji asubuhi ya leo, nao walikuwa wakinunua vitu dukani. Ndipo mama mmoja akasema, "Kuna mama upande wa pili wa barabara hapa, kutoka kwangu, mume wake ana biashara huku. Alikuwa kwenye mkutano ule, kule, hivi majuzi usiku. Naye

alikuwa na kitu fulani mguuni mwake, nacho kilikuwa ni... Mtu huyo mimbarani alikuwa akimwambia mwanamke huyo juu ya kitu hicho, na unajua kiliondoka, nalo lilimsisimua kupindukia."

Binti-mkwe wangu alisema, "Huyo ni baba mkwe wangu." Kasema, "Huyo ni baba mkwe wangu." Kasema, "Je, umekuwa huko?"

Kasema, "Loo, la, nisingeweza kwenda."

Kasema, "Vema, kwa nini usiende huko?"

Akasema, "Mume wangu ni shemasi wa moja ya makanisa makubwa hapa mjini, nisingeweza kwenda karibu na kundi la watu kama hao."

Binti-mkwe wangu akasema, "Lakini umekaribishwa kuja kwa vyovyote vile."

131 Halafu mnazungumza kuhusu madhehebu! Mbona, mnapiga kelele juu ya Mkatoliki! Mbona, wewe ni kitu kile kile, unaona, ni sawa kabisa; sufuria haiwezi kusema nyungu ni nyeusi. Mnajua hiyo ni kweli. Mbona, ni jambo lile lile, hasa, kwa sababu Mungu mmoja si ndiye Baba yetu sote?

132 Kwa nini madhehebu yetu yatutenganishe? Kwa nini mhudumu fulani, mwenye digrii fulani ya chuoni, ajaribu ku—kumzuia mwanamke, ambaye kweli anahitaji uponyaji katika mwili wake, kutoka mahali fulani na kuponywa na Mungu ambaye yeye anadai kwamba anamjua? Hilo ndilo linalonishangaza.

Ndugu, maskini malkia huyo aliangalia huku na huku na kusema, "Lakini nimekuwa nikisikia juu ya haya yote, lakini sijawahi kuona chochote bado."

"Vema, kama ukienda, tutakutenga."

133 "Vema, afadhali unipe makaratasi yangu sasa, kwa sababu ninaenda." Mnaona, Kristo anapoanza kutembea moyoni, imekwisha. Ni hayo tu. Kwa hiyo kumbukeni alikuwa na mengi ya kumkabili, alikuwa na mengi. Sasa, alipoteza uanachama wake.

134 Na jambo lingine, alilosema, nilifikiri lilikuwa zuri sana, alisema, "Ikiwa jambo hilo ni kweli, linafaa kuungwa mkono." Basi akakusanya pesa nyingi sana, ubani, dhahabu, fedha, na manemane, akaviweka juu ya ngamia. Lakini hili hapa wazo lake, naamini, "Ikiwa ni ukweli, nitaiunga mkono; ikiwa si kweli, ninaweza kurudisha hazina zangu mara moja." Angeweza kuwafundisha Wapentekoste jambo fulani, wanasaidia huduma za redio, huku nje, ambazo zingefanya mzaha na kucheka dini ile ile mnayoiwakilisha, hiyo ni kweli, na kanisa lenu wenyewe likiteseka kwa ajili ya zaka ambayzo mngeninii...mnapaswa kuyapa, naam, bwana, kwa sababu tu wana namna fulani ya jina kubwa ama kitu kama hicho.

135 Je, hamjawahi kujifunza mambo ya kiroho bado? Inatupasa. Hiyo ni kweli. Tunapaswa kupambanua roho kuona inakotoka. Sasa, hayo si machunda, sasa, kama unaweza kuyayeyusha.

136 Angalieni sasa, maskini mwanamke huyu, yeye alisema, "Nitaiunga mkono ikiwa ni ya kweli. Ikiwa ni—ikiwa ni ya kweli, inastahili kila kitu, ikiwa si ya kweli, haifai hata kidogo." Kwa hiyo angeweza kurejesha zawadi zake.

137 Sasa kumbukeni, alikuwa na safari ndefu, wala hangeweza kusafiri . . . Ilimbidi kuvuka Jangwa la Sahara, si kwa Kadilaka iliyoyoyozwa, bali juu ya mgongo wa ngamia. Mnajua inauchukua msafara huo muda gani kutoka pale alipokuwa mpaka Palestina? Iliwachukua miezi mitatu, siku tisini, juu ya mgongo wa ngamia. Si ajabu Yesu alisema atafufuka katika Siku ya Hukumu na kukihukumu kizazi hiki. Watu wengine hawatavuka barabara kuona jambo lile lile. Kweli.

138 Na jambo lingine, kumbukeni, wana wa Ishmaeli walikuwa wanyang'anyi jangwani. Naye alikuwa na kikosi kidogo tu cha askari, matowashi. Ni rahisi jinsi gani wangeweza kumshambulia, na kuwaua maskini hao matowashi, na kuchukua hazina zake, na kuendelea.

139 Lakini unajua, ikiwa umedhamiria kumwona Mungu, Mungu atakufanyia njia, wala hakuna hofu hata kidogo juu ya chochote. Una fanaka moja tu, wazo moja, nia moja, lengo moja, na hilo ni "Kumfikia Mungu." Na kama Mungu alisema nawe, utaenda, sijali kinachotukia. Mungu atakuandalia njia ya kufanya hivyo, kama kweli umetia nanga na unajua unachozungumzia. Naye alifanya hivyo.

140 Akawakusanya wajakazi wake na matowashi wake na wote wakapanda ngamia. Naye akasafiri, labda, usiku, kulikuwa na joto sana jangwani. Ninaweza kuwazia wakati wa mchana, huku ameketi chini ya kivuli mahali fulani, kwenye oasisi ndogo chini ya miti fulani, akichukua Magombo hayo na kuyasoma apate kuona. Alitaka kujua, alipofika kule, kama ilikuwa ni ya Kimaandiko.

141 Basi alipokuja, hakuja kama wengi wetu tunavyofanya hapa. Tutahudhuria mkutano mara moja, "Ya jirani . . . Nina jirani mwema, anayeishi hapa chini, walitualika, na kwa hivyo tutaenda huko. Nitakaa dakika tano, na kama akisema jambo moja ambalo ni kinyume na kile ninachoamini, nitasimama moja kwa moja na kuondoka." Hilo linaonyesha ujinga, hilo hata halionyeshi akili timamu. Mtu yeyote aliyelelewa vizuri asingefanya jambo kama hilo.

Kama niliingia kwenye hekalu la Buddha, kama niliingia kwenye hekalu, ningekuwa muungwana vya kutosha kuketi pale mpaka angalau mkutano huo umalizike. Hiyo ni kweli.

142 Mnanena juu ya baadhi ya ujinga wa Kentucky, mnanena juu ya jimbo hilo ninalotoka, ujinga wa hao watu huko chini, sijui.

Wakati mwingine nashangaa. Acha mmoja wa binti zao aingie asubuhi huku nywele zake zimejaa matimutimu, na rangi za makucha usoni mwake, usiku kucha amekuwa na maskini Riki na mtindo bapa wa kukata nywele, Nawaambia, ataninii—atajua wakati mwingine anapotoka . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kipande cha mwanzi, ama kijiti cha mhikori pale, na kumcharaza kwelikweli.

143 Nami nawaambia, ninyi nyote mnanena juu ya kutowajibika kwa vijana, kuna magazeti mengi sana yanayolizungumzia. Nafikiri ni kutowajibika kwa wazazi. Ikiwa ungalikuwa na ile *Kanuni ya Msingi* ya kale imening'inia ukutani pamoja na amri kumi zimetundikwa juu yake, umpeleke kijana huko nje, na kumchapa kidogo, hungekuwa na matatizo mengi hivi. Na kusema, "Maskini mtoto Riki, wewe ni mzuri. Hakumaanisha kufanya makosa, Martha." Anahitaji kucharazwa kwelikweli, ndiko anahitaji.

Biblia ilisema, "Usipoitumia fimbo, unamharibu mtoto wako," na hiyo ni kweli kabisa. Kamwe hutapata jambo bora zaidi.

144 Nyumbani kwangu walikuwa na Amri Kumi zikining'inia, juu ya mlango, kwenye kijiti cha hikori cha urefu *huo*, na, ndugu, nilikuwa na yote kumi mgongoni mwangu, na juu na chini miguuni mwangu, karibu kila siku; ilinifaidi hata hivyo.

Nami nakuambia, Baba alinipeleka nje nyuma ya nyumba, nami nikacheza yosayosa kidogo, lakini nilijua kutofanya hivyo tena, alipomalizana nami.

145 Ingekuwa ni bora zaidi, kama, kama tungekuwa na akina baba wengine wa kufanya hivyo siku hizi. Hakupata kunipiga kiboko kimoja ila kile ambacho mimi namheshimu, usiku wa leo, kwa ajili yake. Nilipotazama ndani ya lile jeneza, na kuona mvi zake kando ya kichwa chake, nilisimama pale nayo machozi yakadondoka usoni mwake, nikasema, "Baba, nilichangia kuyaweka hapo. Mungu anisaidie." Hiyo ni kweli. Nilimheshimu baba yangu, alikuwa baba ambaye angenifanya nitende mema. Naam, bwana. Tunahitaji wengine kama hao siku hizi.

146 Sasa, yeye akaja, akasimama mbele ya—ya ikulu. Akapakua shehena za ngamia wake, kisha akawaweka wajakazi wake hapo chini, akapiga hema zake, naye alikuja kukaa mpaka aliposhawishika. Loo, ndugu, si ajabu atakihukumu kizazi hiki. Um-hum, um-hum. Alikuja kukaa mpaka aliposhawishika, naye akangoja.

147 Sasa, asubuhi ya kwanza, ninaweza kusikia tarumbeta zikilia, kengele zikilia, naye maskini malkia huyo akavaa nguo, akaingia, na labda alikuwa, akachukua kiti kule nyuma kabisa. Basi kila kitu kiliendelea vizuri, uimbaji wote, nayo kwaya yote ikaimba. Ndipo Mchungaji Sulemani akaingia mimbarani.

Naye akaona, ajabu jinsi gani! Maskini moyo wake ukaanza kuwaka moto. Vema, siku hiyo, labda kwenye kibanda cha vitabu, hapana shaka alinunua vitabu hapo. Akarudi huko nje usiku huo, akasoma, na kusoma. Kesho yake, yeye . . . siku baada ya siku . . .

148 Hatimaye kadi yake ya maombi iliitwa; hata hakulipuka kuhusu hilo, alingoja hadi zamu yake. Ndipo ilipofikia mahali aliposimama mbele ya Sulemani, Biblia ilisema kwamba hakuna neno alilofichiwa Sulemani ila alilomfunulia. Amina. Sulemani, roho ya upambanuzi ilimwambia siri za moyo wake. Yesu alisema kwamba malkia huyo atasimama katika Hukumu na kukihukumu kizazi hicho kuwa kimekosa, maana aliye mkuu kuliko Sulemani alikuwepo pale.

149 Angalieni alichosema. Tunafunga. Angalieni alichosema, alisema, "Yote niliyoyasikia yalikuwa ni kweli, na zaidi ya yale niliyosikia." Mnaona, mwujiza ulikuwa umefanyika juu yake wakati huo. Mnaona, alikuwa ametoka huko mbali sana Sheba, naye alikuwa Myahudi hapa juu, na kwa hiyo hakujua lolote juu yake, lakini aliposimama mbele zake, alifunua siri zote za moyo wake, akamwambia mambo ambayo alitaka kujua. Kila kitu kilichokuwa moyoni mwake, Mungu alimjulisha Sulemani.

150 Je, hamwoni? Mungu yeye yule . . . Ungewezaje kuiita telepathia? Ungewezaje kuiita ibilisi? Loo! Wakati hutambui kwamba ninasimama hapa, huku najua unachowazia huko nje! Unawezaje kutilia shaka? Vipi . . . ? Watu wangu wana shida gani? Nini . . . ? Hivi hamwezi kumwona Mungu yeye yule ni asili ile ile, kote kote katika Biblia kila mahali?

151 Naye akageuka, akasema, "Heri watu walio pamoja nawe, wanaosimama hapa na wanaweza kuona karama hiyo kuu ya Mungu ikifanya kazi kila siku. Ni heri jinsi gani haya macho yanayoketi na kuyaona."

152 Yesu alisema, "Atasimama kwenye ile Hukumu na kukihukumu kizazi hiki kuwa kimekosa; kwa maana yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa."

153 Na, marafiki Wakristo, angalieni, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani, Roho Mtakatifu Mwenyewe yupo hapa. Kristo katika umbo la Roho Mtakatifu yuko pamoja nasi, akithibitisha kwamba ile ile, hata ile Sulemani alikuwa nayo, ila tu imeizidi mara nyingi, iko hapa leo, pamoja na miaka elfu mbili na mia tano ya historia ya Roho yeye yule akifanya kazi Kanisani. Hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

Moyo wake uliguswa, hakuwa ameona kitu chochote hapo awali, halikuwa la kawaida kwake. Alijua ilikuwa ni ya kweli.

154 Hebu niseme jambo fulani hapa, kwa muda kidogo tu. Wakati watu, watu halisi wa kweli wanapoweza kuona kitu halisi, kinabadilisha maoni yao. Hiyo ni kweli. Na kwa

kweli, walimwengu wengi siku hizi wana hamu ya kuona kile tunachokataa. Hiyo ni kweli. Wanataka kuona kitu halisi.

155 Hadithi hii ndogo, huenda ikawa na manufaa sasa hivi, nataka kuisimulia. Nyinyi, nyinyi nyote mnajua kwamba mimi huwinda. Mimi—mimi ni . . . Napenda kuwinda. Upande wa mama yangu, amefariki hivi majuzi tu, alikuwa, karibu, nusu-Mhindi. Nami ni—nimewinda maishani mwangu mwote. Kitu cha kwanza nilichowahi kununua, niliokota mimea ya viazi vitamu siku nzima nikapata robo, nikajinunulia mtego wa chuma, kisha nikamkamata sungura, nikamwuza huyo sungura kwa senti kumi na tano, kisha nikajinunulia mitego mingine miwili ya chuma, nikaanza biashara mara moja. Nilikuwa na umri wa miaka sita tu, nimekuwa nikiwinda, nikitega, tangu wakati huo. Nami napanda kwenye misitu ya kaskazini kuwinda, nilizoea, huko juu, na huko juu sana.

156 Nami nilikuwa na mwindaji mwenzi mzuri huko juu, naye alikuwa mwindaji hodari, mwenye shabaha sana, pia mtu ambaye haikukubidi kuwa na wasiwasi juu ya kumpoteza mwituni; alijua jinsi ya kutoka huko. Nami nilikuwa napenda kuwinda pamoja naye, lakini alikuwa na moyo katili sana. A—alikuwa na macho kama mjusi, mwajua jinsi macho hayo ya kuchekesha, kama vile wanawake wanavyojaribu kupaka macho yao rangi siku hizi? Mnajua, macho kama ya mjusi. Na kwa hiyo yeye . . .

157 Alikuwa mtu mzuri sana, lakini alikuwa katili. Alikuwa na mazoea ya kuwaua watoto wa kulungu kunifanya tu nijisikie vibaya. Alikuwa tu . . . Alijua mimi . . . Sasa, ni sawa kumwua mtoto wa kulungu, hiyo ni kweli. Kama sheria inakuruhusu kumwua mtoto wa kulungu, ndugu zangu wawindaji, hiyo ni sawa. Ibrahimu alimchinja ndama na kumlisha Mungu, naye Mungu akamla. Hiyo ni kweli. Kwa hivyo jinsia, au ukubwa havina uhusiano wowote nalo. Lakini kuua tu kiholela, huyo ni mwuaji, mimi siamini katika kuharibu vitu. Nilikuwa mlinzi wa wanyama kwa miaka saba, kama mjuavyo. Kwa hiyo sasa, kumbukeni, daima kuwa mwaminifu na mkweli katika mambo hayo. Na hapa kulikuwa na . . .

158 Angewapiga risasi watoto hawa wa kulungu, na labda hata asiwaokote, kunifanya tu nijisikie vibaya, mwenye moyo katili tu. Nami nilijaribu kuzungumza naye kuhusu Mungu, nami ningemtaja Mungu, angesimama tu hapo na kucheka huku amekirudisha kichwa chake nyuma. Kwa hiyo, lakini chini kabisa ndani yake niliwazia kulikuwa na kitu kizuri ndani ya mtu huyo. Wewe huna . . . Kamwe usimkatae mtu kabisa, jaribu tu uwezavyo, endelea. Acha Mungu amkatae.

159 Kwa hiyo mimi—mimi . . . Siku moja nilipanda huko juu, na huo msimu ulikuwa umeendelea sana. Na hao kulungu wenye mkia mweupe kule juu, jamani, unanena kuhusu Houdini

kuwa bingwa wa kutoroka, alikuwa ni mwanagenzi, kando yao, na kwa vyovyote vile, wakiisha kurushiwa risasi, walikuwa, wanatoweka tu. Na usiku wa mbalamwezi, wangekula usiku, na kutambaa vichakani mchana, wakirudi kichakani; huwezi kuwapata.

160 Ndipo kukaja theluji nzuri, ndogo usiku huo, kama inchi sita ama nane, hali nzuri ya hewa ya kuwafuatilia wanyama. Nasi tulikuwa . . . tukatoka kwenda kuwinda. Basi sikuzote tungebeba chupa ya themosi iliyojaa chokoleti ya moto, kama tungegeukia mahali fulani msituni, au kuua kulungu, ikatubidi kurudi nyuma, ama tukanaswa kwenye dhoruba ya theluji, chokoleti hiyo ilisaidia kukuweka hai. Ni bora kuliko kahawa au chochote kile, kwa sababu ina ma—mafuta ndani yake, na lishe, hiyo chokoleti. Kwa hivyo nilikuwa na . . . Sisi, kila mmoja wetu, alikuwa na robo katika shati letu na sambusa.

161 Nasi tulikuwa tumetembea asubuhi nzima, hata hatukuona mburuzo mmoja, na tulikuwa . . . yapata mwendo wa saa tano na nusu au saa sita, tulifika kwenye uwazi mdogo, yapata ukubwa wa jengo hili hapa. Naye a—alikuwa mbele yangu, akitembea, na kwa kawaida tungeenda juu sana katika . . . juu ya mpaka wa msitu, halafu tungeninii . . . angejitenga, ndipo mmoja angechukua njia moja na mwingine, na kushuka kupitia. Na kama tungempata kulungu, tungemtundika, na tunajua (Tunaporudi kwenye kambi ya chini, tungerudi kule usiku huo, ama kama hatukuwepo, hatukuwa na wasiwasi mmoja juu ya mwenzake, tunajua jinsi ya kujisetiri msituni.), nasi tungerudi kesho yake.

162 Kwa hiyo basi, nilifikiri alikuwa akijiandaa kuondoka, maana tulikuwa tukipanda juu sana. Nao kulungu kwa kawaida hukimbia juu ya mlima wakishikwa na hofu. Na kwa hiyo basi akasimama mahali hapa padogo akaketi chini. Nami nikawazia alikuwa akinyoosha mkono nyuma katika shati lake ashike chupa hii ya themosi ku—kula chakula chetu cha mchana, halafu tungetengana na kurudi. Kwa hivyo badala ya hilo, alitoa maskini filimbi hii.

163 Alikuwa ametengeneza filimbi ndogo iliyolia kama mtoto wa kulungu akimlilia mamaye. Mnajua jinsi—mnajua jinsi mtoto wa kulungu aliavyo, kelele hiyo ndogo ya kipekee. Vema, alikuwa amejitengenezea filimbi, iliyosikika kama huyo kabisa. Ndipo nikamwambia, kabla hatujaondoka asubuhi hiyo, nikasema, “Bert, hutaitumia hiyo.”

164 Akasema, “Ala, wewe ni kama wahubiri wengine wote. Hutawahi kuwa mwindaji, wewe ni mwoga sana.” Kasema, “Usininii . . . ” Kasema, “Wewe ni . . . Nyie wahubiri ni waoga sana hamwezi kuwa wawindaji.” Na kwa kawaida ilinibidi kumwulia wanyama wake kwa vyovyote vile.

165 Lakini—lakini hata hivyo, yeye—yeye alikuwa anataka kumpiga risasi kulungu huyu mdogo. Kwa hiyo akanyoosha mkono wake kwenye shati lake, akatoa filimbi hii, nikasema, "Hutafanya hivyo."

Akasema, "Loo, jirudie, Billy; jirudie." Palikuwa na chungu ya theluji hapo, naye akapiga filimbi hii ndogo.

166 Nami nikawazia, vema, hatukuwa tumeona mburuzo, haingedhuru chochote, lakini nikashangaa, karibu yapata urefu wa jengo hili, kulungu mkubwa mno, mzuri, mwenye mkia mweupe akasimama. Sasa, huyo ni mama kulungu, kulungu jike. Masikio yake makubwa yamesimama namna *hiyo*, macho yake makubwa mazuri yakiangalia. Kulikuwa na shida gani? Haidhuru alikuwa amefichika vizuri jinsi gani, mtoto mchanga, mtoto wake alilia, alikuwa katika dhiki. Akaruka juu, akaanza kutazama pande zote. Sasa, hatukuwa tumesimama zaidi ya yadi thelathini kutoka kwake.

167 Akaniangalia kwa macho hayo ya mjusi, nikawaza, "Loo, jamani!" Naye akaipiga tena, naye kulungu huyo akatoka akaingia moja kwa moja kwenye uwazi huo. Sasa, yeyote anayewinda kulungu anajua hilo si kawaida kabisa. Hawatafanya hivyo, hasa sana wakati wamerushiwa risasi, na wakati huo wa mchana pia, yapata saa tano, saa sita. Aliingia moja kwa moja kwenye huo uwazi.

168 Nami nikamwangalia, nikaanza kuwazia, "Huyo mama, yeye anamdanganya, anapiga filimbi kama mtoto mchanga anayelia, mtoto wake. Naye si mnafiki, yeye haigizi kamwe, hajifanyi, lakini amezaliwa mama, ni silika iliyo ndani yake. Yeye ni mama, na huyo ni mtoto analia." Alikuwa ni aliyezaliwa kuwa mama halisi, ilikuwa ndani yake.

169 Akatoka hapo tena. Akanitazama tena *hivyo*. Nilitikisa kichwa changu *hivyo*. Yeye. . . mimi. . . akanyoosha mkono. Nikasikia risasi hiyo ikipanda katika hiyo .30-06, risasi kubwa ya kizio cha mia moja themanini ya risasi ya uyoga, imelengwa na darubini hiyo, nilijua katika dakika chache alipogusa kifyatulio hicho, alikuwa mwenye shabaha sana, nilijua angeulipulia mbali moyo wake mwaminifu kupitia kwake.

170 Na, "Angewezaje kufanya hivyo?" Nikawaza, "Mtu mwenye moyo katili kama huyo, angeweza kumchukua huyo mama pale, akijaribu kumtafuta mtoto wake, huko nje akimtafuta mtoto wake mchanga, naye angeulipua moyo wake mwaminifu kutoka kwake." Nikawaza, "Ni jamaa katili jinsi gani. Hakika hatafanya hivyo."

171 Ndipo wakati hi—hilo komeo liliposhuka kwenye muundo 70, lilipokashuka namna *hiyo*, huyo kulungu akaisikia, naye akageuka, naye akamwona huyo mwindaji. Lakini je, alisogea? La, bwana. Kwa nini? Alikuwa mama. Afe asife, mtoto wake

alikuwa mashakani, alikuwa akijaribu kumtafuta mtoto huyo. Yeye, akiangalia kila mahali, mtoto alikuwa akiita. Asingeweza kujizuia, alikuwa mama.

172 Ni—ni—ni—nilikuwa karibu kulia, nikageuza tu kichwa changu, nikawaza, "Mungu, siwezi kuona hilo. Anawezaje kufanya hivyo, kuulipua moyo wa maskini mama huyo huko nje, naye amesimama akimtafuta mtoto wake mchanga? Onyesho la kweli la uaminifu, naye anawezaje kufanya hivyo?" Akalenga chini namna *hiyo*, mshipa huo thabiti. Nikageuza mgongo wangu, nami nikasema, "Baba wa Mbinguni," chini moyoni mwangu, "usimruhusu afanye hivyo. Usimruhusu alifanye. Anawezaje kufanya hivyo? Anawezaje kuulipulia mbali moyo wa mama huyo, huku akijaribu kumtafuta mtoto wake mchanga namna hiyo?"

173 Nami nikasubiri, na bunduki haikufyatuka, nikangoja zaidi kidogo, bunduki haikufyatuka. Nami nikageuka kuangalia, na *hivi* ndivyo mtutu wa bunduki hiyo ulivyokuwa ukienda, ukitikisika tu. Ndipo akaangalia juu, huku machozi yakitiririka mashavuni mwake, midomo yake ikitetemeka, akaichukua hiyo bunduki akaitupa, chini kwenye lundo kubwa la theluji, na kunishika kwenye mguu wa suruali, akasema, "Billy, nimetosheka. Niongoze kwa Yesu huyo unayezungumza habari Zake."

174 Yeye ni shemasi katika kanisa la Kibaptisti sasa. Papo hapo kwenye chungu hiyo ya theluji, nilimwongoza kwa Kristo. Kwa nini? Aliona kitu halisi, aliona kitu ambacho hakikuwa ni cha kujifanya, aliona kuna kitu kilicho halisi. Alijua kulikuwa na kitu fulani nyuma yake. Alikuwa mama, alikuwa mama wa kuzaliwa.

175 Mungu, nifanye Mkristo kama huyo, nifanye kuwa Mkristo, ili niweze kuwa halisi sana kwamba watu, ambao wanatafuta kitu halisi, wanaweza kuona kitu halisi, na kujua kwamba Kristo ni halisi.

176 Na tuinamishe vichwa vyetu. Ni wangapi humu ndani... Iweni waaminifu. Hebu kidogo, sivyo? Iweni waaminifu. Ni wangapi kati yenu wangependa kuwa aina ya...Mkristo, kadiri kulungu huyo alivyokuwa mama? Inua mkono wako, useme, "Ni mimi, Ndugu Branham. Na—na—nataka kuwa Mkristo wa namna hiyo." Mungu akubariki.

177 Baba wa Mbinguni, sikujua jinsi gani, nikisimama pale kwenye hiyo theluji siku hiyo, huku miguu yangu imelowa maji, yule mtu amenishika kwenye miguu huku akikoroma na kulia...Vema, nadhani huyo kulungu bado yuko pamoja na mtoto wake mchanga, natumaini. Hakujua hata kidogo alichokuwa akifanya.

178 Lakini Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya. Mtu huyo mwenye moyo katili aliona kitu halisi. Alikuwa ameona

sana imani ya kujifanya na maigizo, kwa, kwa kuwa yeye mwenyewe ni mwindaji, ilimbidi Mungu kumshughulikia kwa njia hiyo, aone ya kwamba kulikuwa na kitu ambacho kilikuwa halisi. Na kama bado anaishi leo, Mkristo wa kupendeza, aliyezaliwa mara ya pili, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hilo, Baba.

179 Niliona mikono mia tatu au mia nne, mia tano, labda karibu na hiyo, labda zaidi ya hiyo, ikiinuliwa juu muda mfupi uliopita, kwamba wao—wao walitaka kuwa Mkristo halisi, Bwana. Imenilazimu kukemea juma hili, Mungu, kulia juu yake, nikishangaa tu kile ndugu zangu wanawaza, nikishangaa Wewe unawaza nini. Nimejaribu kuwa mwaminifu, Bwana. Watu waliketi na kushangaa. Jalia yote yaishe sasa, Bwana. Jalia tu yote yavunjwe na kusuluhishwa. Jalia tumjie Mungu tunayejua kwamba ni halisi. Kila mmoja wetu anaweza kuwa na uzoefu huo wa kuwa Mkristo halisi aliyezaliwa, kadiri tu kulungu huyo alivyokuwa mama. Tujalie, Bwana. Utusikie, naomba.

180 Sasa kila mmoja, huku umeinamisha kichwa chako, macho yako yamefumbwa, nataka useme tu moyoni mwako, omba tu maombi mafupi, "Mungu, unirehemu." Hiyo ni kweli. Amini tu, usiwe na shaka.

181 Ee Mungu! Kila mmoja wenu anayehisi kwamba Kristo yuko karibu nawe, inua tu mkono wako, useme, "Na—naamini tu Yeye yuko karibu nami sana, usiku wa leo, ninauhisi tu Uwepo Wake." Mungu awabariki. Endeleeni tu kuomba. Hilo ni sawa. "Mungu, natamani kuliona." Kuwa tu na imani, amini. "Nifanye Mkristo, Bwana, kama tu . . . Mkristo tu kadiri yule—kadiri yule kulungu alivyokuwa mama."

182 Ni wangapi hawajawahi kuwa mkutanoni hapo awali? Inua mkono wako, hujawahi kuwa mkutanoni. Vema, Mungu awabariki, wengi. Inueni vichwa vyenu kwa dakika moja, kama mmemaliza kuomba, ninawatakeni mwangalie huku.

183 Nilizungumza juma hili juu ya Yesu aliye hai. Sikuwaambia kutoka kwenye katika kanuni ya imani, nimewaambia kwa Biblia, kwa Neno Lake, nimetoa ahadi Yake, ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo? Sasa, kama Yeye . . . Kama ungeweza kuona kitu halisi, ungekitaka, sivyo? Usininii . . . Hutaki kitu chochote cha uwongo, unataka kitu halisi.

184 Mungu na awaonyeshe, usiku wa leo, papa hapa, ya kwamba nimewaambia kweli, Yeye ni Masihi, aliye hai. Msitie shaka sasa, aminini. Angalieni huku na kusema moyoni mwako kwa Kristo, "Wewe ndiwe yule Kuhani Mkuu, ninaamini." Kumbukeni, hebu nilielezee waziwazi: mimi siye Kuhani Mkuu, mimi ni ndugu yenu tu, Yeye ndiye Kuhani Mkuu. Mguso wangu hautakuwa na maana yoyote, mguso Wake utalitekeleza. Mguso wako ndio anangojea Yeye, mguso wako, mguso wako wa imani. Na kama

alifanya hivyo katika siku Zake, atafanya tena leo hii. Hivi hamwamini hilo?

185 Yule mtu, anayeketi *pale*, akiwa na shinikizo kuu la damu, mkono ukiwa kwenye taya yake, unaamini kwamba Mungu atakupa uponyaji wa hilo shinikizo kuu la damu, Bwana? Unaamini? Inua mkono wako, useme, "Nitaukubali." Simjui mtu huyo, lakini hiyo ni kweli.

186 Mwanamke anayeketi karibu nawe *hapo*, ana ugonjwa wa kike pia. Ikiwa ataamini kwa moyo wake wote...Unaamini, Dada? Inua mkono wako.

187 Je, hilo ni jambo halisi? Huyo ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Mwanamke yule ambaye angeweza kugusa, *kule* nyuma, kwa mambo ya udhaifu wake, mwanamke huyo aligusa pia. Kamwe usitie shaka, amini.

188 Mama anayeketi papa *hapa*, ana kansa. Anaiombea kansa yake. Pia ana m—mjukuu anayemwombea, huyo mjukuu amedumaa. Unaamini ya kwamba Mungu ataponya? Hatufahamiani. Ikiwa hiyo ni kweli, punga mikono yako namna *hii*.

189 Sasa, kwa nini hamkuwa na aina hiyo ya imani jana usiku, ninyi nyote? Aminini tu, msitie shaka. Weka mkono wako juu ya mama huyo aliye karibu nawe. Je, utanifanyia fadhili? Anaugua ugonjwa wa koo. Amini tu.

Mnaona jinsi ilivyo rahisi kama mtaamini tu? Usiwe na shaka, amini tu kwa moyo wako wote. Je, Yeye si ni mwema na wa ajabu? Je, hiyo si ni halisi?

190 Mwanamume anayeketi papa *hapa*, anasumbuliwa na matatizo, ana ugonjwa wa tumbo, ugonjwa wa ini.

Mungu, usimwache aukose.

191 Bw. Brines, amini. Umeupata. Ni tamu sana sasa. Usi—usifanye lolote la kulikatisha, liache liendelee. Simjui mtu huyo, sijawahi kumwona. Mungu Mbinguni anajua hilo, na hii hapa Biblia yangu juu ya moyo wangu, angeweza kuniua dakika hii.

192 Amegusa nini? Alimgusa nani? Yeyote yule aliyekuwa hapo, endapo hatufahamiani, hatufahamiani, inua mkono wako, hata mtu huyo awe nani. Yeyote wa hao watu walioitwa, kama hatufahamiani, inua mkono wako. Hatufahamiani. Inueni mikono yenu, yeyote aliyekuwa watu hao, ambao wameitwa sasa hivi, uh-huh, hakika. Mnaona?

193 Vipi kuhusu mtu fulani *huku*? Mama anayeketi *hapo*, akinitazama moja kwa moja, anahofia mno juu ya hiyo kansa. Anashangaa, unashangaa kama ni wewe, "Je, ni mimi, ndiye unayezungumza naye?" Nitakwambia ni nani, jina lako ni Bibi Brown. Sasa, unajua ninazungumza na nani sasa. Unaamini ya kwamba Mungu amekuponya? Kama unaamini, inua mkono wako, useme, "Ninaikubali." Mungu akubariki.

194 Huyo mlevi sugu unayemwombea, amini. Ulijaribu kwa moyo wako wote, lakini haikufanikiwa vizuri. Lakini usijali, Yeye anajua kuhusu hilo. Sasa, kama hiyo ni kweli, punga mkono wako *hivi*. Hakuna anayejua hilo ila wewe na Mungu na mimi. Nilijuaje ulichokuwa ukiombea? Huna budi kuamini. Huna budi kuwa na imani, usiwe na shaka.

195 Huyo mama mweusi, anayeketi hapo karibu nawe, kutoka Portland, um-hum, naam, unaamini kwa moyo wako wote? Bibi Beck, unaweza—unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima pia, Yesu Kristo alikuponya. Amina.

196 Unaamini kuna jambo halisi hapa, usiku wa leo? Ni nani? Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Je, huamini hivyo? Sasa, kama unataka kuwa Mkristo halisi, niamini. Ningewezaje kusimama hapa? Roho Mtakatifu angewezaje kufanya kazi namna hii, kupitia hapa, hadi . . . kupitia mnafiki? Mnafikiri Mungu angemheshimu mnafiki? La, bwana.

197 Hakika nilipata dhana Yake ya ishirini- . . . miaka thelathini na mmoja ya huduma, kuzunguka dunia mara saba. Hakika kuna kila namna ya . . . Mungu asingeruhusu hilo. Ninawaambia ukweli, enyi marafiki. Hii ni kweli. Na ni kweli kabisa.

198 Sasa, najua ni sasa hivi . . . Ni—nimepita kwa mbali. Nilikuwa nikitaka, niliwaambia, kuziita kadi za maombi. Lakini ni karibu saa nne. Si—sijui muda huenda wapi, nasikitika kuwaweka hivi. Niliahidi nisingefanya hivi. Ninajaribu kuliondokea tu, kwa dakika moja tu.

199 Kwa hiyo anisaidie, Mungu wa Mbinguni anajua ni kweli, Malaika huyo wa Mungu, unayemwona kwenye picha hiyo, yuko sasa hivi, papa hapa, jukwaani. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Angalieni kitu halisi, aminini. Ikinilazimu kusimama hapa, kesho alasiri, mpaka jua litue, hadi saa nne kesho usiku, nitamwombea kila mtu anayetaka kuombewa, aliye na hizo kadi, endapo hamtaniacha kuwaweka muda mrefu sana, usiku wa leo.

200 Nashangaa jambo fulani. Nitawaulizeni tu swali. Kila mmoja wenu anayejua ya kwamba wewe si Mkristo sana kadiri yule mama alivyokuwa . . . kama yule kulungu alivyokuwa mama, huku ukiona kitu fulani usoni mwako hapa . . .

201 Niliona jambo fulani likitukia pale pale tena, yule mwanamke anayeketi papo *hapo*.

202 Huyu *hapa* mtu mwenye tatizo hilo la tezi dume, akiamka usiku. Mungu akubariki, ndugu, imekwisha. Sasa, inazunguka tu kila mahali, inaenda tu kila mahali. Wakati mimi . . . Wakati yule asiyeamini alipoona jambo halisi, alikuwa tayari kutubu, papo hapo.

203 Nashangaa, usiku wa leo, kama hatungeweza kuwa na ibada nzuri ya kuweka wakfu sasa hivi. Hebu niwaombee

ninyi kwanza, mahali mmeketi. Hebu niombee leso hizi. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

204 Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono yangu juu ya leso hizi, nikizibariki katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao. Mungu, waangalie hawa. Na, Baba wa Mbinguni, kuna wagonjwa wengi huko nje kwenye kusanyiko, kuna wengi wanaoombea wapendwa wao, ninaweza kulihisi, kuliona. Wanaona kuna jambo fulani linaloendelea, Bwana.

205 Ninazidi kuwa dhaifu, dhaifu wakati wote, ninaomba, Mungu, nisaidie. Sasa, nisaidie kuwaombea maombi ya imani, Mungu. Waliketi hapa na kuteseka kutokana na joto, wengi wao walipitia magumu. Usi—usiwaache waikose usiku wa leo, Mungu. Uko hapa kulitekeleza, jalia waone ni kweli.

206 Baba Mungu, siku moja kulikuwa na mvulana mdogo akichunga kondoo wa baba yake. Tunamjua kama Daudi. Aliwajali kondoo wa baba yake, alipewa wajibu wa kuwaangalia hao kondoo, naye hana budi kuwachunga, hakuna hata mmoja wao anayepaswa kupotea, naye simba akaingia na kumchukua mmoja.

207 Maskini Daudi hakuwa na bunduki kubwa, alikuwa na kombeo tu, bali alikutumaini Wewe. Akaenda mbele, akamchukua yule kondoo mdogo ambaye simba huyo alimchukua. Akamwua huyo simba, na kumrudisha huyo kondoo kwenye malisho ya kijani kibichi, akamlaza karibu na maji matulivu, kwa sababu alikuwa ni kondoo wa baba yake.

208 Mpendwa Baba wa Mbinguni, usiku wa leo magonjwa kama vile ugonjwa wa moyo, kansa, kifua kikuu, vilema, hao pepo wa simba wameingia na kuwachukua baadhi ya kondoo Wako, wanawakokota nje. Wamejikokota kupitia kila ofisi ya daktari na kliniki, anawakokota akiwatoa nje, ninawafuatilia, usiku wa leo, Bwana.

209 Sina kitu ila kombeo hili dogo la maombi, lakini Wewe uliahidi, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo." Hao ni kondoo Wako, nami ninawafuatilia.

210 Ewe shetani, itakubidi, kuwaachilia, ninawarudisha, usiku wa leo, kupitia maombi ya imani. Waachilie, na uwaachilie, ninawadai kwa ajili ya Bwana Mungu. Katika Jina la Mwanawe, Yesu Kristo, mshiko wako wa kutokuamini na uvunjike kote katika jengo hili na kila mmoja wao aponywe.

Tujalie, Baba, katika Jina la thamani la Yesu.

211 Usitilie shaka, amini. Je, unaamini hilo? Inua mkono wako, useme, "Ninaamini, Ndugu Branham, ninaamini." Kama Mungu anaweza kusimama hapa na kutumia kwa ajili ya hili . . . Hivi Yeye pia hakusema, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo?" Uliitumia kwa njia zote . . .

212 Sasa, ni wangapi hapa ndani, wasiomjua Mungu, nao wanataka kuwa Mkristo, inua mkono wako. Sema tu, "Ninataka kuinua mkono wangu, Ndugu Branham, ninataka kuwa Mkristo." Ni washiriki wangapi wa kanisa hapa, ambao wanajua kweli kwamba wewe huishi jinsi unavyopaswa kuishi, kuna mambo ambayo huwezi kuyaelewa kamwe, ume—umechanganyikiwa kabisa, hujui la kufanya, nawe ungependa kweli kuwa Mkristo wa kweli? Inua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham." Mungu akubariki.

213 Ninashangaa, tunapoimba wimbo, ikiwa mpiga kinanda wetu atatupa sauti, "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza," Nashangaa, wote tu wanaoamini ya kwamba Mungu angesikia maombi yangu, nawe unamhitaji Mungu kwa ajili ya hayo, si uje na kusema, "Ninayasalimisha maisha yangu, nafsi, naona kitu halisi, kitu ambacho kimetoka kwenye Biblia, halisi, nami naja, usiku wa leo, na kusimama kwenye madhabahu, ninakuja kuchukua msimamo wangu, sasa hivi. Na tangu siku hii na kuendelea, basi Mungu nisaidie, nitayaweka wakfu maisha yangu Kwake. Nitakuwa mshiriki bora katika kanisa langu, nitakuwa Mkristo aliyejitolea zaidi. Tangu saa hii na kuendelea nauza kila kitu cha ulimwengu, nitakuwa Mkristo halisi, tangu saa hii na kuendelea, kwa neema ya Mungu. Naja, Ndugu Branham, kusimama hapa, nataka uniombee"?

214 Je, utakuja, huku tukiimba? Njoo, inuka moja kwa moja uje. Mungu akubariki, huyo . . . Hata uwe nani, njoo sasa hivi. Ndivyo hivyo. Kujiweka wakfu, ndicho tunachotaka.

> Nampenda (Unampenda Yeye kweli? Nafsi
> yako ni kitu kwako sasa?), . . . mpenda
> Kwani . . .

215 Nataka kujaribu kupeana mikono na wengi niwezao. [Ndugu Branham anaacha kipaza sauti ili kupeana mikono na wale waliokuja kuzunguka madhabahu; maneno yake hayatambuliki—Mh.] . . . ? . . . Simameni hapa madhabahuni, pamoja.

216 Je, hutashuka, uyaweke wakfu maisha yako? kama wewe ni Mkristo, wala kamwe huishi, katika ushindi, kama unavyopaswa, unajua kama Yesu angekuja usiku wa leo, usingekuwa tayari kwenda, ungehofu kungekuwa na kasoro fulani. Kama ungeenda nyumbani, hapa, uanze kwenda zako barabarani, nawe usikie moyo wako ukizimia, ingembidi daktari kuangalia mapigo yako, aseme, "Uh-oh, siwezi kusaidia. Umeenda."

217 Vipi ikiwa ni ajali, na damu ianze kutoka, unahisi moyo wako ukisogea, uko chini ya gari, umebanwa? Loo, unatamani ungekuja. Imechelewa sana wakati huo, njoo sasa. Usibahatishe wakati wowote, marafiki, njoni.

218 Sasa, hebu niwaambie, hamtawahi kuona chochote kilicho halisi zaidi kutoka kwa Mungu, hata mtakapomwona Yesu uso kwa uso, maana hivyo ndivyo hasa Yeye alivyofanya alipokuwa hapa. Naye angelifanya hivyo tena, kama angalikuwa amesimama hapa, wakati siku hii ikiendelea. Si uje?

Napenda . . .

Kila mtu aimbe. Hebu tuinue mikono yetu.

. . . nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

219 Siku moja utamtaka aseme, "Imefanywa vyema, mtumishi Wangu mwema na mwaminifu. Atakayeungama dhambi yake . . . "

220 "Lakini kama nikiwaza uovu moyoni mwangu, basi Mungu hatayasikia maombi yangu," alisema Daudi. Uovu ni nini? Uovu ni jambo ambalo unajua kwamba unafanya ambalo hupaswi kufanya na bado hutatubu. Kama nikiwaza uovu moyoni mwangu, nikijua ya kuwa ninapaswa kulifanya, nisilifanye, basi Mungu aliahidi, Biblia inaahidi kwamba Mungu hatayasikia maombi yako, kama unajua unapaswa kufanya hivyo wala hutafanya. Hiyo ni kweli, ndugu? Hiyo ni kweli, ndugu wahudumu? Ni kweli, "Ukiwaza uovu . . . "

221 Sasa, kama wewe ni mfuasi wa makanisa haya, unasema, "Vema, huyo *hapo* amesimama mchungaji wangu, anaamini mimi ni Mkristo." Kweli. Njoo ujiweke wakfu. Mchungaji wako atafurahia hilo, hakika atafurahia, atafurahia kujua. Anajua unyofu halisi, na shauku ya moyo wako ni kufanya yaliyo mema. Ninayo . . . Kama lingekuwa kanisa langu, hakika ningefanya hivyo. Nanyi ndio kanisa langu, dunia nzima ni parokia yangu, kwa hiyo ninyi ni kanisa langu. Sasa, kama uko hapa, nawe unataka kuyaweka wakfu maisha yako, tunapoimba mara nyingine tena kisha tutaomba, njoo sasa.

Nampenda, . . . mpenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari . . . (. . . ? . . .)

222 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tukivumisha . . . ? . . . Nitaingia miongoni mwa watu hapa chini sasa. Kila mtu akiomba. Sasa, njoo hapa. Sasa, jambo pekee unaloweza kufanya ni kukiri kutoka moyoni mwako, kukiri kwamba umekosea na kuamini.

223 Sasa, Mungu alikuona ukitembea hapa, Yeye hana kikomo, anajua yote juu yake. Naye alikuona ukitembea huku, Yeye Ndiye aliyezungumza nawe, aliujua moyo wako, alinena nawe ukaja mbele. Anakuona sasa hivi. Kiri kwamba umekosea,

useme, "Mungu, samahani nilifanya hivyo. Nisaidie usiku wa leo, Bwana, nataka unisamehe. Kwa neema Yako nitasimama mwaminifu Kwako hadi mwisho wa dunia, nitakuwa mtumishi Wako." Sasa, hebu kila mtu katika kusanyiko ainame na kuomba.

224 Ee Mungu, Baba yetu, tunakikaribia Kiti Chako cha neema. Wamesimama kuzunguka madhabahu hii, usiku wa leo, baadhi yao wamesimama, kundi kubwa la watu. Wengi wao ni washiriki wa makanisa. Baadhi yao labda hawajawahi kuungama bado; baadhi yao wamefanya hivyo na kushindwa. Lakini, Mungu, najua una imani na mtu, ambaye wakati anapojaribu, anashindwa, na kisha ni askari kutosha kusimama kwa miguu yake na kujaribu tena.

225 Mungu, ninaomba ya kwamba utajibu kila moja ya haja zao. Wamesimama hapa sasa, vichwa vyao vimeinamishwa, mioyo yao imeinamishwa, wanakuamini Wewe. Wewe ni Mungu wao. Wanakiri kuwa wamekosea, na wa—wanataka kuwa sawa, Bwana; wanataka kutokuamini kwote kuondolewe kwao. Acheni dhambi ndogo iwazingayo ambayo inawasumbua kwa urahisi, na iondolewe kwao, usiku wa leo, isirudi tena.

226 Ninasihi kwa ajili ya kila mmoja wao. Uliwatazama walipoinuka kutoka kwenye kiti chao, wakishuka kutoka kwenye roshani, wakishuka kutoka kwenye marefu ya kanisa. Unasema, "Naam, hiyo . . . Ningaliweza kusimama hapo nyuma na kufanya vile vile." Mungu, wito wa madhabahuni ulikuwa uje hapa, na hilo lilionyesha ya kwamba hawakuona haya kukiri kwamba wako makosani. Nao wamekuja, wakiungama mbele za Mungu na Malaika watakatifu, wakikiri mbele ya wanadamu wenzao, ya kwamba wamekuwa makosani, na wanataka kuwa sahihi. Walipopanda kuja hapa, kutembea kwao hapa kwenyewe kulifanya maungamo yao.

227 Sasa, Wewe uliahidi ya kwamba watasamehewa, nami ninajua wamesamehewa, Bwana. Nami ninawaelekeza Kwako sasa, kama mtumishi Wako, katika maombi mafupi, nikiamini, nikihisi moyoni mwangu Roho Mtakatifu mkuu amefurahishwa na yale waliyofanya.

228 Nami naomba, Mungu, ya kwamba wataishi maisha ya ushindi siku zao zote zilizosalia, siku zao zilizosalia ziweze kujaa ushindi. Jalia Shetani, jalia magonjwa, yawaache, jalia pasiwe na jambo lolote litakalowasumbua, na jalia wakutumikie Wewe siku zote za maisha yao. Na siku moja, kama ukikawia, nao wakashuka kwenye saa ya kufa, nazo maskini zile pepo kali baridi zianze kupenya kando ya kitanda, au mivuke baridi ya Yordani ikipitia usoni mwao, tunajua kwamba ile Meli ya Kale ya Sayuni itapiga filimbi yake nayo itakuja na kumchukua msafiri huyo kumvusha mto. Tujalie, Bwana. Wafikishe kwenye—kwenye Nchi ya ahadi salama.

229 Wape Uzima wa Milele, Bwana, na uwafufue katika siku za mwisho. Tujalie, Bwana. Jalia, kesho, kila mmoja wa washiriki hawa wa kanisa aende kanisani mwao akiwa na uso unaong'aa na ushuhuda wa utukufu wa Mungu, kwamba wamepata Nanga mpya, usiku wa leo, na sasa wao ni Wakristo waliojitolea kwa ajili ya huduma Yako.

230 Katika Jina la Yesu ninawakabidhi Kwako kwa maombi yangu. Na, Ee Bwana, ikiwa nimepata neema machoni Pako, umtwae kila mmoja wao, ninawakabidhi Kwako kwa moyo wangu wote, katika Jina la Yesu.

231 Sasa, wale, walio karibu na madhabahu hapa, ambao mmekuja kufanya maungamo yenu ya kwamba mmekosea, na mnaamini ya kwamba Mungu anawasamehe, nawatakeni, mwinue mikono yenu namna hiyo. Inua mkono wako, useme, "Najisikia moyoni mwangu kuwa Mungu amenisamehe, na tangu usiku huu na kuendelea naahidi kwamba nitamtumikia Mungu vyema zaidi siku zangu zote."

232 Sasa, ninawatakeni, mgeuke moja kwa moja, kwa wasikilizaji, geukeni tu moja kwa moja, ninyi nyote madhabahuni, geukeni moja kwa moja kwenye kusanyiko, moja kwa moja *hivi*. Sasa, inueni mikono yenu tena, kulielekea kusanyiko, na kumwambia huyu, "Niombee." Semeni pamoja nami, "Niombee." Wote hao...Watu wanaosimama hapa, rudieni nyuma yangu, [Wale walio madhabahuni wanarudia nyuma ya Ndugu Branham—Mh.] "Niombee, ili niwe mwaminifu kwa Mungu kila wakati. Ninajua, ndugu, dada, ya kwamba nitamtumikia Mungu, na ninatamani maombi yako."

233 Sasa, ninyi nyote huko nje, mtakaofanya hivyo, inueni mikono yenu, na kusema, [Kusanyiko linarudia nyuma ya Ndugu Branham—Mh.] "Ndugu na dada yangu, ninaahidi maombi yangu na msaada wangu kwako, upendo wangu na uaminifu wangu, kama ndugu na dada yangu. Mungu, nisaidie kufanya hivyo. Amina."

234 Sasa, sisi sote huku tumeinua mikono yetu kwa Mungu...

Nampenda, nampenda...

235 (Sawa, mchungaji, kumbukeni ibada za kesho. Samahani kwa kuchelewa, waambie kwamba nitamshughulikia kila mmoja wao, ikibidi nibaki hadi usiku wa manane kesho usiku.)

Tazama, Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa SWA62-0721
(Behold, A Greater Than Solomon Is Here)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumamosi jioni, tarehe 21 Julai, 1962, kwenye Ghala la Silaha la Taifa huko Salem, Oregon, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org